**Serikali** yabanwa bungeni kuhusu madeni wazabuni na makandarsi



UKURASA 5

**Wabunge** wataka kushushwa bei ya umeme kukamilika Bwawa la Nyerere



UKURASA 5

**Sakata** matibabu NHIF Aga Khan laibua mjadala

UKURASA 7


# Nipashe

Jumamosi Agosti 31, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581785

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





**RONALDO: NITARUDI KUCHEZEA UEFA**

UKURASA 22




# Mvutano mwingine wa polisi, CHADEMA

UKURASA 2

## Sheria Ulinzi Mtoto yaweka kibano makosa ukatili kingono

UKURASA 3



Dk. Omary Ubuguyu

# Maradhi ya figo yabebesha serikali mzigo wa gharama

• **Mtaalamu** abainisha bil. 80/- hutumika matibabu kwa mwaka... *Endelea Ukurasa 4*

**MICHEZO** **GAMONDI: HATUJACHEZA VIZURI** UK.24

**MAONI,** UK.6



Madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila kwa kushirikiana na Mtaalamu bingwa wa magoti kutoka hospitali kubwa nchini India ya Yashoda, Dk. Ram Mohan Reddy wakimfanyia upasuaji wa goti mmoja wa wagonjwa wakati wa kambi ya siku tano, hospitalini hapo, juzi. PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE

# CHADEMA na polisi zaingia mvutano mpya

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Jeshi la Polisi vimeingia katika mvutano mpya baada ya kuwapo madai kuwa chama hicho kimepanga kufanya maandamano na kuvamia vituo vya polisi.

Wakati polisi ikidai hivyo, CHADEMA imeibuka na kulitaka jeshi hilo kuweka hadharani madai hayo kama kuna ushahidi.

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi hilo, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, ilisema maandamano hayo yamepangwa kwa kile alichokita kuwa baada ya CHADEMA kutoridhishwa na uamuzi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam.

Kutokana na madai hayo, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje CHADEMA, John Mrema, alisema wameichukulia kauli hiyo kwa uzito mkubwa.

"Agosti 10, mwaka huu, polisi walitoa kauli kama hiyo wakati vijana wakijiandaa kuadhimisha siku ya vijana mkoani Mbeya na baada ya kauli hiyo kutolewa na Kamishna Awadhi viongozi wetu walianza kukamatwa na wengine kuumizwa vibaya," alisema.

Mrema alidai kuwa kauli hiyo hawawezi kuiacha kubaki hata kwa dakika moja kwa sababu ni ya uongo.

"Ni kauli ambayo ni hatari na kuhatarisha usalama wa viongozi na wanachama wa CHADEMA. Kwa sababu tangu hukumu ya mahakama hakuna kikao chochote kilichofanyika kwa njia ya zoom au kawaida, hata kikao cha sekretarieti juzi hakikufanyika kwa sababu tulikuwa tumetawanyika nchini," alisema.

Kutokana na hilo, Mrema alisema CHADEMA inalitaka Jeshi la Polisi lithibitishe kwa sababu ni jaribio la kunyanyapaa viongozi wa chama hicho kufanywa kama wahalifu wakati hicho si chama cha kihalifu.

"Tunalitaka Jeshi la Polisi litoe ushahidi hadharani. Hatujafanya kikao chochote achilia mbali kupanga haya ambayo wanasema yamepangwa. Tunalaani kauli hii ya Jeshi la Polisi kwani ina nia ovu dhidi ya viongozi na wanachama," alisema.

Alisema kauli hiyo wanaoona kama ni mkakati wa Jeshi la Polisi kuvuruga vikao vya ndani vya CHADEMA, ambapo wanajiandaa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Wanataka watuvuruge tusiweze kuandaa wagombea, tusiandae mawakala kwa ajili ya uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura na mawakala wa Daftari la Wakazi,"

"Tatu, tunalitaka Jeshi la Polisi watekeleze amri ya mahakama ya kuwarejesha kina soka mtaani, utekaji ni uhalifu kama mwingine.

"Mahakama imewapa amri waitekeleze, badala ya kutafuta visingizio kuwa CHADEMA wanaandaa vijana kuvamia vituo vya polisi. Kama polisi linaogopa vijana 20 basi lifumuliwe na kusukwa upya," alisema.

Mrema alisema wanawataka wanachama wao wasiingie hofu na kama kuna tatizo la kipolisi wasisite kwenda vituo vya polisi na wanategemea watapewa huduma kama wananchi wengine.

"Kauli hii ya Jeshi la Polisi inawatisha wanachama wetu kwenda vituo hivyo hata kama wana jambo la kipolisi kwa kuhofia kukamatwa. Jambo la tano, Jeshi la Polisi liache tabia hiyo kuwaona viongozi na wanachama CHADEMA kama wahalifu. Polisi ifute kauli yake mara moja.

"Tunatoa wito kwa Amiri Jeshi Mkuu (Rais Samia Suluhu Hassan) alifumue Jeshi la Polisi na kulisuka upya, kwani intelejensia yake imedhibitika imefeli tena kama ilivyofeli awali, Mbeya.

Mrema alilitaka Jeshi la Polisi kuacha kufanya kazi kwa kile alichokiita, kutumia ramli ambayo ni chonganishi.

"Kama kuna mtu Jeshi la Polisi wanadhani anawapa taarifa za CHADEMA, anazidi kuwadanganya na kuwadhalilisha, ndio maana wanakurupuka na kutoa taarifa zisizo za ukweli," alidai..

**MADAI YA POLISI**

"Mahakama ilitoa uamuzi wake kuhusiana na shauri lililowasilishwa mbele yake ikiwamo kutoa amri kwa Jeshi la Polisi kufanya upelelezi kujua mahali walipo viongozi wa Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA) Wilaya ya Temeke.

"Viongozi hao ni Deusdedit Soka na wenzake wawili. Jeshi la Polisi lilipokea amri hiyo na kuongeza nguvu katika upelelezi ambao lilishaanza toka awali baada ya kuripotiwa kwa viongozi hao," alisema.

DCP Misime alidai kuwa baada ya uamuzi huo wa mahakama, Jeshi la Polisi limepata taarifa za uhakika za viongozi wa CHADEMA kufanya kikao kwa njia ya kieletroniki (zoom) na kukubaliana kwa vile hawajaridhika na uamuzi wa mahakama kwa sababu hayakuakisi malengo yao.

Kwa mujibu wa Misime, CHADEMA wamekubaliana waanze kuhamasisha wafuasi wao chinichini kufanya maandamano ya kuelekea maeneo mbalimbali pamoja na maofisini.

DCP Misime alidai kuwa wamekubaliana wahamasishe na kuunda vikundi vya vijana wapatao 20, ili wavamie vituo vya polisi vilivyoko jijini Dar es Salaam kwa wakati mmoja.

"Jeshi la Polisi linatoa onyo kali kwa yeyote atakayeendelea kuratibu, kuhamasisha na kushiriki katika uhalifu huo wa kupangwa ambao, lengo ni kutaka kuvuruga amani ya nchi yetu, baada ya kushindwa kwa mikakati yao (atakayefanya hivyo) atashughulikiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Jeshi la Polisi lingependa kusisitiza atakayefika kituo cha polisi kwa nia ovu, tumejiandaa na atashughulikiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria," alisema DCP Misime.

**VIONGOZI WALIOTEKWA**

Alisema baada ya hukumu ya mahakama kutoka, mawakili walitoa tamko kuwa watakata rufani, hivyo wamewaachia waendelee na hilo.

Mrema alidai, "Mahakama wakati huo huo inasema hakuna ushahidi kama wanashikiliwa na Jeshi la Polisi, lakini papo hapo inalitaka Jeshi la Polisi lichunguze, tangu lini mtuhumiwa akajichunguza mwenyewe na kuja na ukweli."

Alisema CHADEMA kinasisitiza Rais Samia kuunda Tume ya Kimahakama ya Majaji kuchunguza tuhuma zote za watu kupotea, kuteswa na kutekwa.

"Leo tunaambiwa watu 10 wamefukiwa kwa mganga. Kama mganga mmoja anaweza kufukia watu 10, fikiria tuna waganga wangapi, ni watanzania wangapi wamepoteza ndio maana tunasisitiza tume iundwe," alisema.

## 'Tuondoe vikwazo vya rufani za tiba'

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametaka watoa huduma za afya wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuondoa vikwazo vinavyozuia wagonjwa wanaotafuta matibabu ndani ya ukanda huo.

Amesema nchi wanachama ikiwamo Tanzania zimejitahidi kuwekeza katika sekta ya afya na kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya kanda kwa matibabu.

Majaliwa alisema hayo jana alipokuwa mgeni rasmi katika Mkutano wa 12 wa Shirikisho la Watoa Huduma za Afya Afrika Mashariki uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Njerere (JNICC), Dar es Salaam.

"Hatua hii ni kwa manufaa ya wananchi wetu na kwa uchumi wa kikanda na ukuaji wa utalii tiba.

"Kwa sasa ni wagonjwa wachache sana wanaosafiri nje ya nchi zetu kwa ajili ya matibabu, kwani karibu magonjwa yote makubwa sasa yanaweza kutibiwa ndani ya Afrika Mashariki," alisema.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alitoa wito kwa wawekezaji wa sekta ya afya kuwekeza nchini Tanzania.

Alisema serikali imetengeneza sera rafiki za uwekezaji hususan katika Sekta ya Afya kutokana na uhitaji wa huduma hizo nchini.

"Tunawakaribisha wawekezaji wote wenye nia ya kuwekeza kwenye sekta ya afya, Sera nzuri tunazo, Sheria na kanuni nzuri tunazo, mahitaji ya uwekezaji kwenye sekta ya afya ni makubwa na tunataka tupate teknolojia mpya na huduma za kibingwa," alisema.

Pia aliwataka wadau wa afya wa kanda kujadili mbinu mbalimbali za kuimarisha mifumo ya afya na kuwa na mikakati ya pamoja ya kukabiliana na magonjwa.

"Tumieni jukwaa hili kuweka mikakati ya pamoja ya kupambana na magonjwa ya mlipuko, magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ambukiza pamoja na magonjwa mapya yanayotokana na mabadiliko ya hali ya tabia nchi," alisema.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema uwekezaji uliofanywa na serikali kuanzia ngazi ya chini umewezesha ugunduaji wa magonjwa yakiwa katika hatua za awali.

"Rufani kwenda nje ya nchi zimepungua kwa kiasi kikubwa kipindi cha nyuma watu waliokuwa wanafika Ocean road walikuwa kwenye hatua za mwisho za ugonjwa, lakini kutokana na uwekezaji sasa zaidi ya asilimia 70 ya wagonjwa wanakuja wakiwa na magonjwa katika hatua za awali," alisema.

HABARI KITAIFA

## Safari mapambano biashara haramu binadamu bado ndefu

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI wa Mtandao wa Kitaifa wa Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Edwin Mugambila, amesema Tanzania bado ina kazi kubwa ya kupambana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu hasa kwenye hoteli.

Mugambila aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa programu maalumu ya kuwajengea uwezo mameneja wa hoteli mbalimbali ili wawe sehemu ya kuzui matukio hayo kuendelea nchini.

Alisema Tanzania imeendelea kuwa chanzo, mkondo na ni mapitio ya usafirishaji haramu wa binadamu na hoteli hazijasalimika.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu Tanzania ni wanawake, wasichana na watoto. "Sehemu mojawapo ambayo wanatumika kunyonywa hawa watoto na wanawake ni sehemu za hotelini na hoteli zinatumika kwa sababu ni ngumu kutambua vile viashiria ndani ya hoteli.

"Tunawajengea uwezo ili waweze kutambua viashiria na kuchukua hatua watafahamu mamlaka za nchi za kutoa taarifa na mwisho wa siku itasaidia kudhibiti vitendo vya usafirishaji ambavyo vinatokea maeneo ya hoteli," alisema.

Aidha, Mugambila alisema nchi ina sheria kali ambazo kama itatokea mtoto anafanyiwa biashara ya kingono ndani ya hoteli adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 hadi kifungo cha maisha jela.

Alisema kuna faini ya Sh milioni 50 hadi Sh. milioni 300 na sambamba na hilo hoteli inaweza kufilisika kwa kutaifisha mali zote za hoteli inapobainika kuwa fedha yote wanayoipata katika hoteli ni mazao ya uhalifu.

Mugambila alisema sheria ya mwaka 2008 imeelekeza nchi inaweza kutaifisha mali zote na wahusika kupelekwa jela na kufungwa kifungo cha kuanzia miaka 30.

"Nitoe rai kwa waendesha hoteli wote kuwa macho ili vitendo hivyo visitokee ndani ya hoteli zao na watumiaji wa hoteli wanapoona viashiria ni vizuri kutoa taarifa ili wanaofanya vitendo hivyo wachukuliwe hatua,"alisema Mugambila.

Alisema watoaji wa taarifa watalindwa kwa mujibu wa sheria za nchi na itasaidia kuwa na taifa salama kuhusiana na vitendo vya usafirishaji haramu wa binadamu.

Aidha, alisema sheria hizo zimeanza kufanyiwa kazi japo kuna changamoto ya utekelezaji wa suala hilo.

"Hatua zimeanza kuchukuliwa japo haziridhishi hazitoshi hatua muhimu zinachukuliwa na tumeona ripoti ya Marekani ya mwaka huu ya usafirishaji haramu wa binadamu imeiweka Tanzania kuwa kwenye msimamo wa pili kwenye mapambano hayo hakuna nchi yoyote ya Afrika ambayo ipo kwenye daraja la kwanza nchi nyingi ambazo zinafanya vizuri zipo daraja la pili,"

Alisema hiyo inaonesha kuwa kama taifa hatua zimechukuliwa lakini bado kuna safari ndefu na kazi kubwa inahitajika ili kuondoa mitandao ya usafirishaji wa binadamu.

Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Michael Battle, alisema ni wakati wa kuwekeza katika mikakati ya kuongeza ulinzi wa haki za binadamu kwa kupamba na usafirishaji haramu.

Alisema serikali ya Marekani inaunga mkono kukuza amani na usalama ambayo ni pamoja na kufuta usafirishaji haramu wa binadamu ambao ni upotezaji mkubwa na ukiukwaji wa utu wa ubinadamu.

Balozi Battle aliwahimiza wamiliki wa hoteli na wafanyakazi wa hoteli kuwa mstari wa mbele katika kugundua na kuripoti wafanyabiashara wa binadamu kwa kuwa wapo katika nafasi nzuri ya kugundua ishara za usafirishaji haramu wa binadamu.

Naibu Kamishna wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ahmad Mwendadi, alisema wanayo mikakati ya kutosha ya kupambana na kuzuia biashara hiyo.

Alisema usafirishaji wa binadamu ni uhalifu kama ulivyo uhalifu mwingine, hivyo kuna sheria ya mwaka 2008 ambayo inakataza vitendo vyote ambavyo vinaashiria usafirishaji haramu wa binadamu.

Naye Meneja Mkuu wa hoteli ya Ramada Resort na Girafe, alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo, hivyo watakuwa sehemu ya kupambana na kuzuia biashara hiyo haramu ya usafirishaji wa binadamu.

# Sheria Ulinzi wa Mtoto yaweka kibano makosa ya ukatili kingono



**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limepitisha Muswada wa Sheria zinazohusu Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 wenye mambo mbalimbali huku ukiweka kibano zaidi kwenye makosa ya ukatili wa kingono kutokana na wimbi la vitendo vinavyochangiwa na kukua kwa teknolojia.

Muswada huo umegusa sheria tatu ambazo ni Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura ya 443; Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 na Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21.

Akiwasilisha maelezo ya muswada huo bungeni jana, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema Kifungu cha 13 cha sheria ya makosa ya kimtandao kimeandikwa upya na kuweka masharti yanayohusiana na makosa ya unyanyasaji na utumikishaji wa kingono kwa watoto kwa kutumia nyenzo za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

"Lengo ni kuwalinda watoto kutokana na kuwepo kwa ongezeko la matukio ya uhalifu wa kingono dhidi ya watoto kupitia nyenzo za TEHAMA zinazotumika kuwashawishi, kuwatishia au kuwaonesha watoto ponografia kwa lengo la kuwashawishi kushiriki katika matendo ya kingono,"alisema.

Alisema yamewekwa masharti yanayozuia mtu au mfumo wa kompyuta kutekeleza kitendo cha kigaidi na kuweka adhabu kwa mtu anayekiuka masharti hayo ili kudhibiti na kuzuia vitendo hivyo vinavyoweza kutendeka kwa njia ya kompyuta au mifumo ya kompyuta.

"Kifungu cha 49 kimeandikwa upya ili kuweka masharti yanayohusu adhabu kwenye makosa yanayotendwa na kampuni au taasisi. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha namna ya kushughulikia uhalifu unaotendwa na kampuni au taasisi na kuhakikisha kuwa wakurugenzi wa kampuni wanawajibika kwa uhalifu wa kimtandao unaofanywa na kampuni au taasisi wanazozisimamia,"alisema.

Aidha, alisema muswada umerekebisha mamlaka ya kufifilisha makosa yasihusishe makosa ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto ili kufanya adhabu kwa makosa ya udhalilishaji wa kingono dhidi ya watoto itolewe na mahakama pekee kutokana na uzito wa makosa hayo.

"Pia tunapendekeza kuondoa dhana ya Shule za Maadilisho na badala yake kuweka dhana iliyokusudiwa ambayo ni Makao ya Malezi ya Watoto waliotoroka kutoka sehemu waliyowekwa kwa amri ya mahakama ya uangalizi baada ya kuondolewa kwenye familia zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uhanga wa ukatili, mazingira hatarishi," alisema.

Kadhalika, alisema muswada umeongeza sharti la ulazima kwa mahakama kuzingatia taarifa ya uchunguzi wa kitaalamu kutoka kwa afisa ustawi wa jamii wakati wa kutoa amri ya kugharamia vipimo vya vinasaba ili kuiwezesha mahakama kufikia uamuzi wa haki na unaotekelezeka.

"Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayomtaka afisa ustawi wa jamii kuandaa taarifa ya uchunguzi kwa ajili ya kutumika mahakamani wakati wa mashauri yanayohusu malezi, matunzo, uangalizi na haki ya kumuona mtoto," alisema.

Alibainisha kuwa lengo ni kuisaidia mahakama kupata taarifa ambazo zitaiwezesha kutoa uamuzi wa haki na unaozingatia maslahi bora ya mtoto.

Alisema muswada unapendekeza kubainisha mamlaka za mahakama katika kushughulikia mashauri ya kuasili watoto. Aidha, mahakama ya watoto inaongezwa miongoni mwa mahakama zitakazoshughulikia mashauri hayo ili kuongeza ufanisi na kupunguza mlundikano wa mashauri katika mahakama nyingine.

"Pia inapendekezwa kuiondolea mahakama mamlaka ya kuruhusu mtoto kusafirishwa nje ya nchi wakati wa utoaji wa amri ya mpito kabla ya kukamilika kwa mchakato wa kuasili mtoto ili kuhakikisha ulinzi kwa mtoto anayekusudiwa kuasiliwa kabla ya mahakama kutoa amri ya kuasili,"alisema.

Muswada huo umeondoa mapendekezo ya kupunguza muda unaotakiwa kwa mwombaji wa kuasili mtoto asiye mtanzania kukaa nchini kutoka miaka mitatu hadi miaka miwili mfululizo.

Pia umerahisisha utaratibu wa uwasilishaji wa maombi ya malezi ya kambo kwa kuondoa mlolongo mrefu uliopo sasa.

Hata hivyo, Kifungu kipya cha 71A kimeongezwa kwa lengo la kuipa mahakama mamlaka ya kufuta amri ya kuasili kwa manufaa ya mtoto baada ya kupokea maombi kutoka kwa mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto aliyeasiliwa au mtu mwingine yeyote mwenye maslahi.

"Marekebisho mengine ni kuongeza muda wa kumlea mtoto kabla ya kumuasili kutoka miezi mitatu hadi miezi sita ili kuwezesha na kurahisisha taratibu za kuasili na kulinda maslahi bora ya mtoto,"alisema.

**MABARAZA YA WATOTO**

Aidha, alisema Muswada huo unalenga kuanzisha na kurasimisha mabaraza ya watoto katika ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na ngazi ya Taifa ili kuwa na majukwaa yanayowafikia watoto na kujua changamoto zinazowakabili ili kuweza kuwalinda na matukio ya unyanyasaji na uhalifu katika jamii.

**KUWALINDA NA UHALIFU**

Kifungu cha 102 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kumlinda mtoto dhidi ya uhalifu kwa kutoruhusu mtoto kuchangamana na wahalifu ambao ni watu wazima hata kama ni ndugu.

"Kifungu cha 103 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti kwa mahakama kuhusu kuharisha kesi zinazowahusu watoto wanaotuhumiwa kutenda makosa ya mauaji,"alisema.

Alieleza kuwa lengo ni kuharakisha usikilizwaji wa mashauri ya watoto na kuwalinda watoto hao dhidi ya kujifunza tabia za uhalifu gerezani.

Vile vile, alisema mtoto anarekebishwa nje ya mfumo wa mahakama kwa makosa madogo ili kumsaidia kubadilika kitabia kupitia mifumo ya jamii iliyopo zikiwamo ofisi za ustawi wa jamii na vilevile kupunguza muda na gharama za uendeshaji wa kesi za watoto.

Aidha, marekebisho hayo pia yanampa Jaji Mkuu mamlaka ya kutengeneza kanuni zitakazoainisha utaratibu wa kuwadodosa watoto mahakamani, huku utaratibu sahihi wa uwasilishaji wa rufaa kutoka mahakama ya mtoto kwenda mahakama kuu na kuondoa utata ukiwekwa.

**WIGO WA MAKOSA**

Pia alisema imependekezwa kupanua wigo wa makosa ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto ili kuongeza ulinzi kutokana na kuongezeka kwa kasi ukatili huo unaochangiwa na kukua kwa teknolojia na utandawazi.

**MAKOSA YA UKEKETAJI**

Pamoja na hayo, alisema Kifungu cha 158A kimefanyiwa marekebisho ili kukifanya kuwa na nguvu dhidi ya masharti ya sheria nyingine kuhusu makosa ya ukeketaji wa watoto na kutoa fidia kwa wahanga wa makosa hayo.

## Safari mapambano biashara haramu binadamu bado ndefu

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI wa Mtandao wa Kitaifa wa Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Edwin Mugambila, amesema Tanzania bado ina kazi kubwa ya kupambana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu hasa kwenye hoteli.

Mugambila aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa programu maalumu ya kuwajengea uwezo mameneja wa hoteli mbalimbali ili wawe sehemu ya kuzui matukio hayo kuendelea nchini.

Alisema Tanzania imeendelea kuwa chanzo, mkondo na ni mapitio ya usafirishaji haramu wa binadamu na hoteli hazijasalimika.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu Tanzania ni wanawake, wasichana na watoto. "Sehemu mojawapo ambayo wanatumika kunyonywa hawa watoto na wanawake ni sehemu za hotelini na hoteli zinatumika kwa sababu ni ngumu kutambua vile viashiria ndani ya hoteli.

"Tunawajengea uwezo ili waweze kutambua viashiria na kuchukua hatua watafahamu mamlaka za nchi za kutoa taarifa na mwisho wa siku itasaidia kudhibiti vitendo vya usafirishaji ambavyo vinatokea maeneo ya hoteli," alisema.

Aidha, Mugambila alisema nchi ina sheria kali ambazo kama itatokea mtoto anafanyiwa biashara ya kingono ndani ya hoteli adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 hadi kifungo cha maisha jela.

Alisema kuna faini ya Sh milioni 50 hadi Sh. milioni 300 na sambamba na hilo hoteli inaweza kufilisika kwa kutaifisha mali zote za hoteli inapobainika kuwa fedha yote wanayoipata katika hoteli ni mazao ya uhalifu.

Mugambila alisema sheria ya mwaka 2008 imeelekeza nchi inaweza kutaifisha mali zote na wahusika kupelekwa jela na kufungwa kifungo cha kuanzia miaka 30.

"Nitoe rai kwa waendesha hoteli wote kuwa macho ili vitendo hivyo visitokee ndani ya hoteli zao na watumiaji wa hoteli wanapoona viashiria ni vizuri kutoa taarifa ili wanaofanya vitendo hivyo wachukuliwe hatua," alisema Mugambila.

Alisema watoaji wa taarifa watalindwa kwa mujibu wa sheria za nchi na itasaidia kuwa na taifa salama kuhusiana na vitendo vya usafirishaji haramu wa binadamu.

Aidha, alisema sheria hizo zimeanza kufanyiwa kazi japo kuna changamoto ya utekelezaji wa suala hilo.

"Hatua zimeanza kuchukuliwa japo haziridhishi hazitoshi hatua muhimu zinachukuliwa na tumeona ripoti ya Marekani ya mwaka huu ya usafirishaji haramu wa binadamu imeiweka Tanzania kuwa kwenye msimamo wa pili kwenye mapambano hayo hakuna nchi yoyote ya Afrika ambayo ipo kwenye daraja la kwanza nchi nyingi ambazo zinafanya vizuri zipo daraja la pili,"

Alisema hiyo inaonesha kuwa kama taifa hatua zimechukuliwa lakini bado kuna safari ndefu na kazi kubwa inahitajika ili kuondoa mitandao ya usafirishaji wa binadamu.

Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Michael Battle, alisema ni wakati wa kuwekeza katika mikakati ya kuongeza ulinzi wa haki za binadamu kwa kupamba na usafirishaji haramu.

Alisema serikali ya Marekani inaunga mkono kukuza amani na usalama ambayo ni pamoja na kufuta usafirishaji haramu wa binadamu ambao ni upotezaji mkubwa na ukiukwaji wa utu wa ubinadamu.

Balozi Battle aliwahimiza wamiliki wa hoteli na wafanyakazi wa hoteli kuwa mstari wa mbele katika kugundua na kuripoti wafanyabiashara wa binadamu kwa kuwa wapo katika nafasi nzuri ya kugundua ishara za usafirishaji haramu wa binadamu.

Naibu Kamishna wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ahmad Mwendadi, alisema wanayo mikakati ya kutosha ya kupambana na kuzuia biashara hiyo.

Alisema usafirishaji wa binadamu ni uhalifu kama ulivyo uhalifu mwingine, hivyo kuna sheria ya mwaka 2008 ambayo inakataza vitendo vyote ambavyo vinaashiria usafirishaji haramu wa binadamu.

Naye Meneja Mkuu wa hoteli ya Ramada Resort na Girafe, alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo, hivyo watakuwa sehemu ya kupambana na kuzuia biashara hiyo haramu ya usafirishaji wa binadamu.

# Sheria Ulinzi wa Mtoto yaweka kibano makosa ya ukatili kingono



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalumu, Dk. Dorothy Gwajima akiwasilisha muswada wa sheria ya marekebisho ya Sheria mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024, bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limepitisha Muswada wa Sheria zinazohusu Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 wenye mambo mbalimbali huku ukiweka kibano zaidi kwenye makosa ya ukatili wa kingono kutokana na wimbi la vitendo vinavyochangiwa na kukua kwa teknolojia.

Muswada huo umegusa sheria tatu ambazo ni Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura ya 443; Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 na Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21.

Akiwasilisha maelezo ya muswada huo bungeni jana, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema Kifungu cha 13 cha sheria ya makosa ya kimtandao kimeandikwa upya na kuweka masharti yanayohusiana na makosa ya unyanyasaji na utumikishaji wa kingono kwa watoto kwa kutumia nyenzo za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

"Lengo ni kuwalinda watoto kutokana na kuwepo kwa ongezeko la matukio ya uhalifu wa kingono dhidi ya watoto kupitia nyenzo za TEHAMA zinazotumika kuwashawishi, kuwatishia au kuwaonesha watoto ponografia kwa lengo la kuwashawishi kushiriki katika matendo ya kingono,"alisema.

Alisema yamewekwa masharti yanayozuia mtu au mfumo wa kompyuta kutekeleza kitendo cha kigaidi na kuweka adhabu kwa mtu anayekiuka masharti hayo ili kudhibiti na kuzuia vitendo hivyo vinavyoweza kutendeka kwa njia ya kompyuta au mifumo ya kompyuta.

"Kifungu cha 49 kimeandikwa upya ili kuweka masharti yanayohusu adhabu kwenye makosa yanayotendwa na kampuni au taasisi. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha namna ya kushughulikia uhalifu unaotendwa na kampuni au taasisi na kuhakikisha kuwa wakurugenzi wa kampuni wanawajibika kwa uhalifu wa kimtandao unaofanywa na kampuni au taasisi wanazozisimamia,"alisema.

Aidha, alisema muswada umerekebisha mamlaka ya kufifilisha makosa yasihusishe makosa ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto ili kufanya adhabu kwa makosa ya udhalilishaji wa kingono dhidi ya watoto itolewe na mahakama pekee kutokana na uzito wa makosa hayo.

"Pia tunapendekeza kuondoa dhana ya Shule za Maadilisho na badala yake kuweka dhana iliyokusudiwa ambayo ni Makao ya Malezi ya Watoto waliotoroka kutoka sehemu waliyowekwa kwa amri ya mahakama ya uangalizi baada ya kuondolewa kwenye familia zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uhanga wa ukatili, mazingira hatarishi," alisema.

Kadhalika, alisema muswada umeongeza sharti la ulazima kwa mahakama kuzingatia taarifa ya uchunguzi wa kitaalamu kutoka kwa afisa ustawi wa jamii wakati wa kutoa amri ya kugharamia vipimo vya vinasaba ili kuiwezesha mahakama kufikia uamuzi wa haki na unaotekelezeka.

"Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayomtaka afisa ustawi wa jamii kuandaa taarifa ya uchunguzi kwa ajili ya kutumika mahakamani wakati wa mashauri yanayohusu malezi, matunzo, uangalizi na haki ya kumuona mtoto," alisema.

Alibainisha kuwa lengo ni kuisaidia mahakama kupata taarifa ambazo zitaiwezesha kutoa uamuzi wa haki na unaozingatia maslahi bora ya mtoto.

Alisema muswada unapendekeza kubainisha mamlaka za mahakama katika kushughulikia mashauri ya kuasili watoto. Aidha, mahakama ya watoto inaongezwa miongoni mwa mahakama zitakazoshughulikia mashauri hayo ili kuongeza ufanisi na kupunguza mlundikano wa mashauri katika mahakama nyingine.

"Pia inapendekezwa kuiondolea mahakama mamlaka ya kuruhusu mtoto kusafirishwa nje ya nchi wakati wa utoaji wa amri ya mpito kabla ya kukamilika kwa mchakato wa kuasili mtoto ili kuhakikisha ulinzi kwa mtoto anayekusudiwa kuasiliwa kabla ya mahakama kutoa amri ya kuasili,"alisema.

Muswada huo umeondoa mapendekezo ya kupunguza muda unaotakiwa kwa mwombaji wa kuasili mtoto asiye mtanzania kukaa nchini kutoka miaka mitatu hadi miaka miwili mfululizo.

Pia umerahisisha utaratibu wa uwasilishaji wa maombi ya malezi ya kambo kwa kuondoa mlolongo mrefu uliopo sasa.

Hata hivyo, Kifungu kipya cha 71A kimeongezwa kwa lengo la kuipa mahakama mamlaka ya kufuta amri ya kuasili kwa manufaa ya mtoto baada ya kupokea maombi kutoka kwa mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto aliyeasiliwa au mtu mwingine yeyote mwenye maslahi.

"Marekebisho mengine ni kuongeza muda wa kumlea mtoto kabla ya kumuasili kutoka miezi mitatu hadi miezi sita ili kuwezesha na kurahisisha taratibu za kuasili na kulinda maslahi bora ya mtoto,"alisema.

**MABARAZA YA WATOTO**

Aidha, alisema Muswada huo unalenga kuanzisha na kurasimisha mabaraza ya watoto katika ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na ngazi ya Taifa ili kuwa na majukwaa yanayowafikia watoto na kujua changamoto zinazowakabili ili kuweza kuwalinda na matukio ya unyanyasaji na uhalifu katika jamii.

**KUWALINDA NA UHALIFU**

Kifungu cha 102 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kumlinda mtoto dhidi ya uhalifu kwa kutoruhusu mtoto kuchangamana na wahalifu ambao ni watu wazima hata kama ni ndugu.

"Kifungu cha 103 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti kwa mahakama kuhusu kuahirisha kesi zinazowahusu watoto wanaotuhumiwa kutenda makosa ya mauaji,"alisema.

Alieleza kuwa lengo ni kuharakisha usikilizwaji wa mashauri ya watoto na kuwalinda watoto hao dhidi ya kujifunza tabia za uhalifu gerezani.

Vile vile, alisema mtoto anarekebishwa nje ya mfumo wa mahakama kwa makosa madogo ili kumsaidia kubadilika kitabia kupitia mifumo ya jamii iliyopo zikiwamo ofisi za ustawi wa jamii na vilevile kupunguza muda na gharama za uendeshaji wa kesi za watoto.

Aidha, marekebisho hayo pia yanampa Jaji Mkuu mamlaka ya kutengeneza kanuni zitakazoainisha utaratibu wa kuwadodosa watoto mahakamani, huku utaratibu sahihi wa uwasilishaji wa rufaa kutoka mahakama ya mtoto kwenda mahakama kuu na kuondoa utata ukiwekwa.

**WIGO WA MAKOSA**

Pia alisema imependekezwa kupanua wigo wa makosa ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto ili kuongeza ulinzi kutokana na kuongezeka kwa kasi ukatili huo unaochangiwa na kukua kwa teknolojia na utandawazi.

**MAKOSA YA UKEKETAJI**

Pamoja na hayo, alisema Kifungu cha 158A kimefanyiwa marekebisho ili kukifanya kuwa na nguvu dhidi ya masharti ya sheria nyingine kuhusu makosa ya ukeketaji wa watoto na kutoa fidia kwa wahanga wa makosa hayo.

## Wabunge wataka kushushwa bei ya umeme

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kupitia upya bei ya umeme baada ya mradi wa kuzalisha umeme wa bwawa la Nyerere (JNHPP) kukamilika ili watanzania wapate unafuu wa huduma hiyo.

Kwa sasa wastani wa bei ya uniti moja ya umeme yenye ruzuku ni sh. 100 (Matumizi ya kawaida chini ya uniti 75 kwa mwezi) na bila ruzuku ni sh. 292.

Aidha, kwa mwananchi anayetumia zaidi ya uniti 75 kwa mwezi, analipa kiasi cha sh.292 kwa uniti moja ikiwa na ruzuku ndani yake badala ya sh. 320.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mbunge wa Lupa (CCM), Masache Kasaka, alisema mradi huo umeanza kutoa umeme wa kutosha na kuna ziada na kuhoji serikali haioni umuhimu wa kupitia ukokotoaji wa bei ya uniti ya umeme ili kuleta unafuu.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alisema gharama za umeme si za uzalishaji pekee bali zinahusisha usambazaji, usafirishaji na uwekezaji.

Alisema kwa sasa bei ya uniti ya umeme imewekewa ruzuku ya serikali ili kupunguza gharama.

Alieleza kuwa bei ya umeme ikilinganishwa na nchi za Afrika Mashariki kwa Tanzania ipo chini na kusisitiza kuwa wataendelea kuchakata na kutoa ruzuku ili wananchi waendelee kupata bei ambayo ni himilivu.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Suma Fyandomo, alihoji lini serikali itashusha bei ya uniti za umeme.

Akijibu swali hilo, Kapinga alisema bei hiyo inapatikana kulingana na gharama za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme.

"Bei ya sasa si halisia ni bei ambayo ina ruzuku za serikali ndani yake ambapo kwa sasa wastani wa bei ya uniti moja ya umeme yenye ruzuku ni Sh. 100 (Matumizi ya kawaida chini ya unit 75 kwa mwezi) na bila ruzuku ni Sh. 292 na kwa mwananchi anayetumia zaidi ya uniti 75 kwa mwezi, analipa kiasi cha sh. 292 badala ya Sh.320,"alisema.

Alisema wataendelea kufanya tathmin ya gharama za utoaji wa huduma za TANESCO mara kwa mara na kuendelea kurekebisha bei kulingana na gharama za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji zitakavyokuwa.

# Serikali yabanwa madeni makandarasi, wazabuni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SUALA la madeni ya makandarasi, wazabuni na watoa huduma kwa serikali limewaibua wabunge na kuitaka serikali kutoa kauli kutokana na baadhi yao kufilisiwa mali zao.

Akiuliza maswali bungeni jana, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Bupe Mwakang'ata, alihoji lini serikali itawalipa fedha wazabuni na wakandarasi waliotoa huduma mbalimbali katika Mkoa wa Rukwa ambao hawajalipwa miaka mitano sasa.

"Makandarasi wengi na wazabuni wamefanya kazi hizi kwa kukopa fedha benki lakini serikali haiwalipi kwa wakati na wengi wamefilisiwa mali zao wameuziwa nyumba na magari yao lini serikali itawalipa?" alihoji.

Pia alisema wazabuni wengi madeni yao yamehakikiwa zaidi ya miezi sita lakini bado hawajalipwa na ni ya muda mrefu kuanzia miaka miwili hadi mitano. Alihoji kauli ya serikali kuhusu wakandarasi hao.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Esther Maleko, alisema tatizo la wakandarasi kutokulipwa limekuwa kubwa hali inayochonganisha serikali na wakandarasi.

"Je, serikali haioni ni wakati wa kumaliza kulipa madeni hayo kutokana na wakandarasi kufilisika?" alihoji.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Cecilia Paresso, alitaka serikali iliambie Bunge ni kwa nini kazi wakipewa makandarasi wa nje wakichelewesshewa malipo yanalipwa na riba na kwa nini makandarasi wa ndani hawapewi malipo na riba.

Akitoa majibu ya maswali hayo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema si kwamba serikali imeacha kulipa kinachojitokeza kumekuwapo na malimbikizo ya madeni ya muda mrefu.

"Tuipongeze serikali ya awamu ya sita imejitahidi sana kulipa madeni haya ambayo mengine yalikuwa na zaidi ya miaka saba, kuna madeni yamelipwa ya tangu mwaka 2013, kwa hiyo huwezi kuyapangia bajeti ya mwaka mmoja yataathiri shughuli nyingine za serikali," alisema.

Alisisitiza serikali itaendelea kuyalipa madeni hayo ya watoa huduma, wazabuni na wakandarasi.

"Utaona mwaka jana ilikuwa takribani Sh.bilioni 400, mwaka huu imefika Sh. bilioni 600 kwa sababu kulikuwa na malimbikizo hayo ndio ilisababisha hali hiyo, msisitizo wa serikali ni kuendelea kuongeza bajeti ya kuwalipa wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ili kutokuathiri shughuli za kiuchumi na mitaji yao,"alisema.

Hata hivyo, alisema bajeti itakayofuata wataendelea kuongeza fedha ili kuhakikisha wanalipa sehemu kubwa na ikiwezekana kuyamaliza yote.

Kuhusu makandarasi wa nje, Mwigulu alisema kuna aina mbili za mikataba kuanzia mikataba inapoingiwa ya ndani na kuna ya nje na kwamba mikataba ya nje makandarasi wengi wanatumia viwango vya kimataifa na wa ndani wanatumia masharti ya ndani.

"Serikali imekuwa ikishawishi mikataba ya nje kutokuwa na riba kwenye mikataba na kwenye mikataba tuliyoingia ya masuala ya kilimo umwagiliaji ili kuepuka gharama za kuchelewa," alisema.

Awali, Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alisema serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni hayo yaliyohakikiwa na kukubaliwa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali.

Alifafanua kuwa kwa mwaka 2023/24, Sh. bilioni 600 zilitengwa kwa ajili ya kulipa madeni hayo na hadi Juni 2024 Sh. Bilioni 491.25 zililipwa.




Mhifadhi misitu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Wilaya ya Ilala, Albert Masao, akitoa elimu kuhusu faida za utunzaji wa misitu kwa viongozi wa vikundi vya kijamii vya Kata za Kivule na Majohe, wakati wa semina iliyoandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Dar es Salaam, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Uharibifu mazingira chanzo afya ya akili

**Na Christina Haule,** MOROGORO

UHARIBIFU wa mazingira umebainika kuwa na nafasi kubwa ya kuchangia mabadiliko ya tabianchi yanayoleta changamoto ya afya ya akili kwa mwanadamu na kumfanya kushindwa kutekeleza majukumu yake kama anavyopaswa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Msaada wa Kisaikolojia, Onesmo Maganga, alisema hayo jana wakati akizungumza katika kumbukizi ya miaka mitano ya Taasisi ya Uhifadhi wa Mazingira na Kilimo (AGRIWEZESHA) iliyofanyika mjini hapa.

Maadhimisho hayo yamebebwa na kauli mbiu isemayo, "Panda Mti, Penda Mti".

Maganga alisema kuna watu wana matatizo ya afya ya akili bila kujitambua na mengine husababishwa na msongo wa mawazo unaotokana na uharibifu wa mazingira, ambao wanahitaji kukutana na mwanasaikolojia.

Alisema mabadiliko ya tabianchi yakitokea husababisha joto kali ambalo likiongezeka mwanadamu anakuwa na msongo wa mawazo sababu joto ni sehemu ya kumpa maumivu ya mwili na kumfanya kupata hasira na pengine kufikia kukumbwa na changamoto ya afya ya akili.

"Pia mkulima anaweza akakosa mazao katika kilimo biashara alichoanzisha kutokana na kukosekana kwa mvua kulikotokana na mabadiliko ya tabia nchi na hivyo, kujikuta akiingia katika msongo wa mawazo na kuangukia katika afya ya akili bila yeye kujua," alisema.

Akizindua Kumbukizi hizo, Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, aliiwataka watendaji wa kata na vijiji kuchukua hatua za haraka kwa wanaoharibu mazingira, kwa kuchoma moto kiholela hasa maeneo ya milimani ili kukomesha kitendo hicho.Nguli aliitaka jamii kuyahifadhi na kuyatunza vizuri mazingira kwa sababu suala hilo lina uhusiano makubwa na maisha ya mwanadamu na anapaswa kutekeleza mambo yake kwa busara, ili kuyalea mazingira ili na yenyewe yamlee.

Aliipongeza AGRIWEZESHA kwa mchango wake mkubwa iliyonesha katika kampeni ya TUTUNZANE, kwa kusaidia kuinua maendeleo ya kilimo, ufugaji na utunzaji wa mazingira.

Mkurugenzi wa AGRIWEZESHA, Deogracia Ignas, alisema tangu kuanzishwa kwake mwaka 2021, taasisi hiyo imeshapanda jumla ya miti 653,200 na inatarajia kupanda miti mingine milioni moja ifikapo mwaka 2025 ikiwamo ya matunda na mbao.

Mkurugenzi huyo alisema wanatekeleza miradi mbalimbali nchini katika kukuza maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla ikiwamo kilimo mseto cha mazao na miti ambapo tayari wamewafikia wakulima zaidi ya 3000.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Timuatimua makocha Ligi Kuu Bara sasa si suluhisho

**WAKATI** Ligi Kuu Tanzania Bara imeingia katika raundi ya pili, tayari 'harufu' ya makocha kutaka kutimuliwa imeanza kusikika hapa nchini.

Hata hivyo kwa upande wa Coastal Union yenye maskani yake jijini, Tanga yenyewe imeshamtupia mkono wa kwaheri aliyekuwa Kocha Mkuu, David Ouma, kwa sababu ya kuondolewa katika mashindano ya kimataifa.

Coastal Union ambayo imeanza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sare ya bao 1-1 ugenini kwa KMC FC, ilifungwa ugenini Angola mabao 3-0 na kulazimisha sare hapa nyumbani waliporudiana katika michuano hiyo inayosimamiwa na kuandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Uamuzi wa kumtimua kocha kwa sababu ya kupata matokeo mabovu unatakiwa kufanyika baada ya viongozi kujiuliza maswali mbalimbali muhimu ambayo yanajiridhisha kutekeleza uamuzi huo na si kwa kuangalia kilichotokea ndani ya dakika 180 za mchezo (yaani dakika 90 za nyumbani na dakika nyingine za ugenini).

Coastal Union ilipaswa kujiridhisha je ilimpatia kila kitu kocha huyo ili naye awapatie matokeo chanya, au ndio imeamua kumtoa kafaya baada ya timu yao kuondolewa katika mashindano hayo ya kimataifa?

Umefika wakati viongozi wa timu, wanachama na mashabiki kuacha tabia ya kuficha mapungufu yao kwa kukimbilia kuwafukuza makocha.

Je ni kweli Coastal Union ilifanya usajili mzuri ambao ulikuwa na uwezo wa kupata matokeo chanya dhidi ya wapinzani wao au iliweka kambi sahihi huku ikitekeleza vyema programu zake za mazoezi kuelekea mechi hizo mbili za kimataifa? Kama majibu ya maswali haya machache ni ndio, basi wanastahili kuchukua uamuzi huo, lakini kama ni tofauti, basi hawakustahili kumpa 'Thank You' kocha huyo.

Ukiondoa Coastal Union, 'moshi' mwingine unaonekana kufukuta kwa upande wa 'Matajiri wa Chamazi' ambao pia timu yao ya Azam FC, iliyaaga mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kufungwa mabao 2-0, ugenini Kigali na wenyeji APR baada ya kuvuna bao 1-0 walipokuwa nyumbani.

Fukuto hilo lilioneka kama halipo au linazimwazimwa kwa kile kilichoonekana timu hiyo ilifanya usajili mzuri na vile vile kuweka kambi Morocco na kucheza mechi mbalimbali za kirafiki, limeibuka tena mapema wiki hii baada ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na JKT Tanzania ambayo inaundwa na wachezaji wazawa pekee.


Kwa kuangalia macho ya nje, ni ukweli usiofichika mabosi wa Azam FC wametumia kiasi kikubwa cha fedha kuwekeza katika kikosi chao na hii ni kwa sababu malengo yao katika msimu huu yalikuwa kufanya vizuri kwenye michuano ya CAF pamoja na mashindano mengine yote watakayoshiriki.

Hata hivyo, mambo yamekwenda tofauti kwa kushuhudia timu yao ikiondolewa kwenye hatua ya awali, lakini tena kidonda kikatoneshwa kwa kushinda kuvuna alama tatu pale ilipowakabili Maafande wa JKT Tanzania.

Kwa viongozi kutochukua uamuzi wa haraka kama ilivyokuwa ikifanya miaka ya nyuma, hii inaonyesha wameanza kukomaa na kuamini mbali na kuipa huduma zote muhimu timu yako, lakini kuna suala la bahati.

Tunazikumbusha kuacha tabia ya kutimua timua makocha kwa kuangalia matokeo ya mechi moja au mbili, kwa kufanya hivyo unaweza kuididimiza timu yako kwa sababu mwalimu mpya atakayeajiriwa naye atahitaji muda wa kuwafahamu wachezaji na wapinzani wao, na hili linaweza kuathiri zaidi timu husika.

Ili timu kupata kushinda makombe inahitaji uwekezaji mkubwa na wa muda mrefu, maandalizi sahihi, kamwe maandalizi ya zimamoto hayawezi kutoa matunda bora, mipango ya muda mrefu ndio njia sahihi ya kujenga vikosi imara na si kubadilisha badilisha makocha kila kukicha.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



# TFF, wamiliki viwanja wekeni huduma rafiki kwa mashabiki

Na Adam Fungamwango

**KWA** nini mashabiki wengi wa soka hawaendi viwanjani? Hili ndilo swali linaloulizwa na viongozi wa soka, waandishi wa habari na hata wachambuzi wa masuala ya mchezo.

Ni kweli kabisa ombwe la mashabiki wengi kutokwenda kwenye viwanja vya soka kuangalia mchezo huo unaopendwa kwa wengi.

Na siyo hawaendi kwa sababu hawaupendi, la hasha. Mpira wa miguu ndiyo mchezo unaopendwa zaidi Tanzania na duniani kote.

Mashabiki wa soka katika nchi mbalimbali za Afrika wamekubali Watanzania wamekuwa na mwamko zaidi kuupenda mchezo wa soka kwa sasa kuliko hata mataifa yao ambapo zamani walikuwa wanatamba.

Ndiyo maana hivi sasa unaweza kuona wachezaji kutoka Cameroon, Mali, Nigeria, Ghana, tena wenye uwezo mkubwa wakija kucheza soka Tanzania badala ya kwenda nchi za Ulaya Mashariki kama ilivyokuwa zamani.

Wachezaji wengi zamani wa Zambia walikuwa hawataki kuja kucheza soka nchini, badala yake walikuwa wakikimbilia Afrika Kusini. Kwa sasa wanamiminika. Sasa kwa nini mashabiki wamepungua sana viwanjani?

Hili limewafanya Bodi ya Ligi na Klabu kuungana na kusaka mshauri ambaye atafanya uchunguzi wa kisayansi ili kupata majibu ya kitaalam.

"Sababu nyingi ambazo watu wanazitoa zinabaki kuwa za kihisia na mhemko tu, sababu ya kitaalam na kisayansi ya kwa nini mashabiki hawaji uwanjani haipo, kwa hiyo ni lazima tuitafute, hivyo Bodi kwa kushirikiana na klabu tutafanya hivyo, sasa tunaipataje? Tumeamua kwa kauli moja kumpata mshauri ambaye atafanya upembuzi yakinifu na uchunguzi," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo.

Kabla hata hawajapata usuari wa mshauri, binafsi nataka kuwapa pa kuanzia ni kwa nini watu wengi hawaendi mpirani siku hizo tofauti na zamani.

Kwanza kabisa picha linaanza kumekuwa na shida ya kuingia milangoni. Milango inafungulia michache bila sababu maalum. Mfano Uwanja wa Benjamin Mkapa ulioko Dar es Salaam una milango mingi na endapo itafunguliwa yote hakuwezi kuwa na foleni kama inavyoonekana. Watu wengi siku hizi hawataki shida wala kusukumana tofauti na zamani ambapo ubabe ilikuwa ni moja kati ya sifa unayotakiwa kuwa nayo ili kuingia uwanjani.

Pili mashabiki wanachukuliwa kama wao ndiyo wanahitaji zaidi huduma ya kuingia viwanjani, badala ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Bodi ya Ligi na Klabu kuwafanya mashabiki kama wateja, au abiria.

Wateja wanapoenda baa, hotelini na kuhudumiwa vizuri kesho watakwenda tena, na hata wakipata huduma nzuri kwenye basi la usafiri, abiria watakuwa wakilitumia mara kwa mara kwenye pale wanapohitaji kusafiri.

Tatizo bado viwanja vyetu vina mindombinu ya kizamani, hivyo hata uingiaji wake uwanjani unakuwa ni wa kama mateso zaidi. Mpaka mtu anaingia uwanjani anakuwa yupo hoi. Ndani hakuna maji, kitafunio, wala viburudisho na vikiwemo vinauzwa bei ya juu kuliko inayouzwa nje ya uwanja.

Kwa wenzetu wameshatoka huko, viwanja vyao vina miundombinu mizuri, mashabiki wakiingia uwanjani wanapata kila kitu ndani, ikiwamo vyakula vinywaji, hivyo kwa watu wengine hupenda kwenda kama mtoko wa familia.

Nadhani TFF, Bodi ya Ligi na klabu zinapokwenda kutafuta chanzo, zianze kwanza kubadisha mtazamo wa mashabiki wa kizamani, siku hizi wanatakiwa kuwabembeleza zaidi ili waje uwanjani, ikiwezekana hata kuweka vinywaji wanavyopenda na kuwauzia ili waweze kujazana. Kama wanaweza kujazana baa wakiwa wanangalia mpira huku wakinywa, iweje viwanjani chini ya usimamizi wa walinzi?

HABARI KITAIFA

## Mbunge aibua sakata la NHIF Aga Khan

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Anatropia Theonest, ameitaka serikali itoe kauli bungeni kuhusu taharuki ya matumizi ya Bima ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwenye hospitali za Aga Khan.

Akiuliza maswali ya nyongeza bungeni jana, Mbunge huyo alisema: "Kumekuwapo na taharuki nchini ya matumizi ya bima ya NHIF kwenye hospitali za Aga Khan. Nini kauli ya serikali kuhusu hatma ya matumizi ya kadi ya NHIF kwa hospitali za Aga Khan ambazo zipo nchini?"

Akijibu swali kwa niaba ya Waziri wa Afya, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, aliwahakikishia wabunge kuwa serikali imeendelea kutoa huduma za afya kupitia NHIF na wanatambua umuhimu wa kuwa na uendelefu wa mfuko.

"Kwa hiyo pamoja na huduma zinazoendelea kutolewa serikali imeendelea kufanya tathmini ili kuhakikisha unakuwa endelevu na huduma zinakuwa na uhakika kwa wananchi.

"Kuhusu hospitali ambayo umeitaja maongezi yanaendelea kati yake, serikali na mfuko wa NHIF ili kuona namna nzuri ya kuendelea kutoa huduma,"alisema.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Segerea (CCM), Bonnah Kamoli, alitaka wanufaika wa bima ya afya ya Toto Afya Kadi kuendelea kuhudumiwa huku taratibu za bima ya afya kwa wote zikisubiri kukamilika.

Dk. Dugange akijibu swali hilo, alisema wanufaika wa Toto Afya Kadi wanaendelea kunufaika isipokuwa mfumo wa kulipia bima za watoto kupitia utaratibu huo umebadilika.

"Kwa sasa usajili wa Toto Afya Kadi unafanyika kupitia utaratibu wa shule na vifurushi vya bima ya afya vya najali, wekeza na timiza ambapo wanajiunga kupitia wazazi wao,"alisema.

Alisema kuanza utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote utawezesha makundi mbalimbali ya wananchi wakiwamo watoto kupata huduma za afya kwa urahisi pasipo kuwa na vikwazo.

# Shehena bandari Dar yafikia makasha 20,150

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imesema shehena ya makasha imeongezeka kutoka 7,151 mwezi Aprili 2024 hadi kufikia makasha 20,151 kufikia Julai, 2024.

Ongezeko hilo linaelezwa kusababishwa na uwekezaji uliofanywa na DP World katika bandari ya Dar es Salaam wenye thamani ya takriban dola milioni 250 kwa ajili ya uendeshaji wa magati 0-7 bandarini.

Meneja wa Shughuli na Uratibu wa TPA, Josephat Lukindo, alisema hayo juzi wakati akiwasilisha ripoti fupi ya utendaji wa bandari hiyo kwa Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzowa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, wakati wa ziara yake badarini jana.

Alisema pesa hizo zimetumika kuboresha utendaji wa bandari hiyo katika maeneo matatu baada ya kukabidhiwa na mamlaka ya bandari Aprili mwaka huu.

"Kwa uzoefu tulionao wa uendeshaji wa bandari, tuliamua kuanza na uboreshaji wa maeneo matatu muhimu ili kuongeza ufanisi zaidi," alisema Lukindo.

Alisema sehemu ya kwanza kampuni ya DP World kupitia kampuni tanzu ya DP World Dar es Salaam iliyoanzishwa kusimamia bandari hiyo ilifanya manunuzi ya mitambo ya kisasa.

Lukindo alisema kampuni hiyo ilifanya ukarabati wa mitambo mibovu iliyokuwa ikitumika bandarini hapo na kufanya manunuzi ya vifaa vipya yakiwamo matrekta 20 ya kubebea mizigo pamoja na matela 31, jenerela saba zenye ukubwa wa KV 10,000 kila moja kwa ajili ya kuendeshea mitambo umeme unapokatika na vifaa vya kubebea mizigo mizito (cranes).

"DP World ilifanya usimikaji wa mifumo ya kisasa ya TEHAMA kwa ajili ya utendeshaji wa bandari hiyo kwa sababu awali tulikuta mifumo ambayo imepitwa na wakati na kuamua kuweka mifumo ya kisasa kuendana na maendeleo ya teknolojia," alisema. Alisema uwekezaji huo wa mifumo ya kisasa umesababisha manufaa makubwa ndani ya kipindi cha miezi mitatu iliyochangia ongezeko la shehena ya makasha ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 18.2.

"Uwekezaji huu utaifanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa katika ushindani na bandari nyingine kubwa barani Afrika ikiwamo ya Morocco," alisema.

Makalla alipongeza utendaji kazi wa TPA na kufurahishwa na mafanikio hayo akielezea kuwa ni kielelezo tosha kwa wale waliokuwa wanaubeza uwekezaji huo.

"Kuna watu wao kazi yao ni kupinga kila kitu hata wakati serikali inanunua ndege walipinga pia na cha ajabu wanafurahia kupanda ndege hizo hivi sasa," alisema Makalla na kuongeza kuwa wengine walipinga uwekezaji wa treni ya SGR na hata ujenzi wa bwawa la Mwalimu Nyerere kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Alisema CCM inaiunga mkono serikali kwa uwekezaji huo katika maeneo yote muhimu ikiwamo bandari kwani hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya CCM.

"Tupo katika ziara ya kutembelea miradi mbalimbali ya uwekezaji iliyotekelezwa na serikali ukiwamo wa Bandari ya Dar es Salaam na kiukweli tumefurahishwa sana na maendeleo tuliyaona," alisema.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Juma Kijavala alisema mafanikio yaliyopatikana ndani ya kipindi kifupi cha uwekezaji wa DP World yametokana na hatua mbalimbali zilizochukua ili kuongeza ufanisi wa utendaji na kuvutia wafanyabiashara zaidi wa ndani na nje ya nchi.

"Bandari ya Dar es Salaam itakuwa na uwezo wa kushindana na bandari nyingine duniani kwa kutoa huduma bora na kwa haraka kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika," amesema Kijavala.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makala (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Juma Kijavara, alipotembelea Bandari ya Dar es Salaam juzi, kujionea uwekazaji uliofanywa bandarini hapo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# LHRC yataka serikali kuridhia mkataba kimataifa ulinzi wanaopotea, kutekwa

**Na Pilly Kigome**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimeitaka serikali kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Watu Wote dhidi ya Kupotea na Kutekwa wa Mwaka 1994, ili kukabiliana na ongezeko la matukio hayo nchini.

Kauli hiyo imetolewa wakati Jeshi la Polisi nchini likishikilia baadhi ya watuhumiwa kutoka mikoa tofauti wanaodaiwa kuhusika na matukio ya mauaji ya watu 10 ambao miili yao imefukuliwa mikoa mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, aliyasema hayo jana Dar es Salaam, wakati akizungumzia Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Waathirika wa matukio ya kutoweka na kutekwa.

Henga alisema serikali inatakiwa iridhie mkataba huo kwa kuwa umeweka taratibu madhubuti za ulinzi wa watu dhidi ya matukio ya utekaji na hatua hiyo itaonesha kujidhatiti katika Jumuiya ya Umoja wa Kimataifa kudhibiti vitendo hivyo.

Dk. Henga aliitaka serikali kupitia vyombo vya ulinzi na usalama, kufanya uchunguzi wa kina wa malalamiko dhidi ya matukio hayo, hususani katika kipindi cha hivi karibuni kwakuwa vitendo hivyo, vinaathiri zaidi watoto, wanawake na jamii yote kwa ujumla.

Alisema Umoja wa Mataifa (AU) uliadhimia na kupitisha mkataba huo ambao unaweka mfumo madhubuti wa kushughulikia ukiukwaji matukio ya utekaji katika Jumuiya ya Umoja wa Mataifa ikiwamo Tanzania.

"Hivyo Tanzania ikiridhia mkataba huo na kuufanya sehemu ya sheria, kufuatia ongezeko la matukio ya utekaji nchini, itakuwa ni sababu tosha ya kuifanya Tanzania kuweka ulinzi thabiti kwa wananchi wake dhidi ya matukio hayo," alisema.

Alisema kwa kuwa Ibara ya kwanza ya mkataba huo inabainisha na kuweka katazo la watu kuwekwa vizuizini na kutekwa kwa kuwa inakwenda kinyume na ulinzi wa ulinzi wa Haki za Binadamu.

"Pia Ibara ya pili inatafsiri vitendo vya kutoweka na utekaji ikijumuisha vitendo vya kukamatwa, kuwekwa kizuizini, kutekwa au namna yoyote ya kumyima mtu uhuru iwe kwa kufanywa na serikali, vyombo vyake, au kwa maelekezo ya serikali kwa kuelekeza chombo au mtu huyo kuficha taarifa za alipo mtu aliyekamatwa au kutekwa.

"Zaidi Ibara ya 3 na 6 ya mkataba huo, inataka mamlaka kufanya uchunguzi wa kuchukua hatua stahiki na kuwafikisha watu wote waliyohusika na matukio ya kufikisha taarifa za mtu aliyetekwa katika vyombo vya kisheria," alisema.

Alisema Ibara ya 24 inaweka sharti kwa mamlaka husika zilizoridhia mkataba huo, kutoa fidia kwa waathirika wote wa matukio ya utekaji ikiwamo kutoa fedha za matibabu, fidia ya madhira pamoja na huduma ya kisaikolojia kwao pamoja na familia zao.

# Ndege ya mizigo ATCL kuanza safari za Comoro

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Ndege Tanzania (ATCL) inatarajiwa kuanza safari za ndege ya mizigo nchini Comoro baada ya kuongezeka kwa mahitaji baina ya wafanyabiashara wa nchi zote mbili.

Safari hizo zitaanza rasmi Septemba 13, mwaka huu, kwa kutumia ndege ya mizigo aina ya Boeing B767-300F yenye uwezo wa kubebea tani 54 za mzigo kwa mara moja na kuruka kwa wastani wa masaa saba hadi 10 bila kutua.

Mkuu wa Kituo cha ATCL Upande wa Comoro, Esther Mahiga, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Balozi wa Tanzania nchini Comoro, Said Yakubu, ubalozini hapo wakati akimtambulisha mwakilishi wa ComAir ambaye ni Wakala wa ATCL nchini Komoro, Kamarouddine Waziri Zamane.

"Hivi sasa ATCL tunafanya safari tatu kwa wiki baina ya Dar es Salaam na Moroni na tunatarajia kuongeza safari hadi kufikia nne kwa wiki. Safari ya nne itakuwa ni ndege ya mizigo B767-309F ambayo tunatarajia kuanza miruko tarehe 13 Septemba, 2024.

"Kuongezwa kwa safari hii ni mwitikio kwa jumuiya ya wafanyabishara wa Tanzania na Moroni ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakiomba huduma ya kusafirisha bidhaa zinazoharibika haraka kutokana na jiografia ya nchi ya Komoro," alisema.

Akizungumza kwenye tukio hilo, Balozi Yakubu alielezea kuridhishwa kwake na huduma ya usafiri wa ndege unaotolewa na ATCL, unaowezesha muunganiko wa safari kati ya Tanzania na Visiwa vya Komoro ambao umeoboreshwa kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita hadi kusababisha mahitaji wa kuanzisha safari za ndege kubwa ya mizigo.

"Mzunguko wa biashara kati ya Tanzania na Visiwa vya Komoro umeongezeka, nasisi tuko tayari kuhakikisha nchi zetu mbili zinaimarisha ushirikiano hayo kwa manufaa ya pande zote mbili", alisema Balozi Yakubu.

Balozi Yakubu alisema kuanza kwa safari za ndege ya mizigo ni ukuaji wa biashara na kuahidi kuwa ofisi yake itaendelea kusaidia shughuli za kiuendeshaji za ATCL ili kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya sita za kufungua nchi kibiashara.

Tangu kuwasili kwa ndege ya kwanza ya ATCL ya mizigo B767-300F mnano Juni 2023, mizigo mikubwa ikiwamo magari, madini, madawa, samani, vipuri na bidhaa zinazoharibika kwa muda mfupi hususan matunda, nyama na mazao ya bahari vimekua vikisafirishwa kutoka na kwenda nchi mbalimbali ndani na nje ya Afrika.

Baadhi ya nchi hizo ni N'Djamena (Chad), Mumbai (India), Dubai (Falme za kiarabu), Nairobi (Kenya), Kinshasha (Kongo), Lusaka (Zambia) na Entebe (Uganda).

## Wakili akwamisha kesi ya wanandoa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeahirisha kesi ya tuhuma ya kujeruhi na kutoa lugha ya matusi inayowakabili wanandoa, Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54), kwa sababu ya kutokuwapo kwa wakili wa washtakiwa kwa taarifa kwamba, yupo Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi.

Kesi ya wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania asili ya kihindi wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana, Dar es Salaam, imeahirishwa hadi Septemba 10 mwaka huu. Wanatuhumiwa kwa mashtaka manne waliyoyatenda Julai 21,2023 kinyume cha sheria.

Taarifa hiyo ilitolewa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Faraja Ngukah, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa mahakama hiyo, Aaron Lyamuya, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa shahidi wa tatu wa upande wa mashtaka.

Wakili Ngukah alidai kuwa kesi ilikuja kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa na walikuwa na mashahidi wawili, lakini wamepokea barua kutoka kwa Wakili wa Utetezi, Edward Chuwa, kwamba ana kesi Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi.

"Yupo kwenye kesi namba 19857/2024 kati ya Agustino Kavishe dhidi ya William Kideme na wengine mbele ya Jaji Hemed, barua hii iliambatanishwa na chamber summons" alidai Wakili Ngukah.

Alidai kuwa kutokana na sababu hiyo, wanaomba wapangiwe tarehe nyingine na Wakili Chuwa amependekeza kwamba, iwe Septemba 10, mwaka huu.

Hakimu Lyamuya baada ya kusikiliza taarifa hiyo, alisema kuwa na wao walipata barua hiyo juzi na amewaonya mashahidi hao waliyokuwa mbele ya mahakama wafike mahakamani, Septemba 10 mwaka huu, kwa ajili ya kutoa ushahidi wao.

Ilidaiwa kuwa Nathwan, anatuhumiwa Julai 21, 2023, akiwa eneo la Mtaa wa Mrima-Kisutu, jengo la Lohana, wilayani Ilala, Dar es Salaam, kinyume cha sheria alimsababishia madhara makubwa Kiran Lalit, kwa kuzamisha kichwa chake katika ndoo ya saruji iliyochanganywa.



Wauguzi wa Hospitali ya Regency, jijini Dar es Salaam, wakihudumia watoto mapacha watatu wa kiume wa raia wa China, Liya Zhang (31) ambaye alijifungua watoto hao, hospitalini hapo usiku wa kuamkia juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## TCRA yaonya TV habari uchochezi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeionya Watetezi TV kwa kurusha habari zinazodaiwa kuwa za kichochezi kupitia chaneli yake ya YouTube.

Amesema kuwa licha ya kituo hicho kuandikiwa barua ya onyo Aprili 5, mwaka huu, lakini kimeendelea kukiuka sheria, kanuni, na masharti ya leseni kwa kurusha tena maudhui yanayokinzana na sheria Julai 30 mwaka huu.

Katika barua ambayo Jambo TV tumeishuhudia, ikiandikwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unaomiliki kituo hicho, TCRA imetaja kauli za Watetezi TV kama ile ya "Serikali imetunyang-anya uhuru wa kupiga kura Ngorongoro, yani ni afadhali hata wafungwa" – Olemangi, kuwa ya kichochezi.

Katiba barua hiyo iliyoandikwa Agosti 23 mwaka huu, TCRA ilisema kuwa tarehe Agosti 12 mwaka huu, Watetezi TV ilirudia kosa lingine kwa kuchapisha maudhui ya namna hiyo kupitia chaneli yake ya YouTube, yenye maelezo "NEC mnavunja Sheria za Uchaguzi" Vijana Ngorongoro watoa msimamo huu, wasisitiza NEC haijatenda haki".

Maudhui hayo yameelezwa kuwa ya upande mmoja wa habari, yakiacha kutoa fursa kwa upande wa serikali au mamlaka husika kutoa maelezo yao kuhusu shutuma zilizotolewa na mwananchi aliyekosoa hali hiyo.

Kwa mujibu wa Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji Mtandaoni 2020, kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022, TCRA ilisema kuwa Watetezi TV imekiuka Kanuni za 9 (a) na 12 (a) (i).

TCRA imeagiza kituo hicho kuondoa mara moja maudhui hayo kutoka chaneli yake na kutoa maelezo ya kwanini hatua za kisheria zisichukuliwe dhidi yao kwa kuendelea kukiuka sheria, huku ikikipa siku saba kutoa maelezo tangu wakati taarifa hiyo ilipotolewa.

TCRA ilisema kuwa endapo Watetezi TV itapuuza au kukaidi kutekeleza maelezo hayo, mamlaka hiyo haitasita kuchukua hatua zaidi za kisheria.



## Mradi wapunguza vifo mama, mtoto

**Na Renatha Msungu,** BAHI

MRADI wa Maendeleo wa AP unaotekelezwa na Shirika la Word Vision Tanzania katika wilaya ya Bahi mkoani hapa, umepunguza vifo vya mama na mtoto kutoka asilimia 80 hadi tano.

Mratibu wa mradi huo, Erick Chalamila, alibainisha hayo jana wakati wa hafla ya kufunga mradi huo uliotekelezwa ndani ya miaka 22 na kuleta matokeo chanya kwenye sekta za afya, kilimo, mifugo na elimu.

Chalamila alisema wanaishukuru World Vision na wafadhili Ireland kutokana na kutoa msaada huo ambao umeibadilisha jamii ya eneo hilo kwenye sekta ya afya, kilimo,ufugaji na elimu.

Alisema hivi sasa wakazi wa Tarafa ya Mundemu wako vizuri kiuchimi ikiwemo mahudhurio mazuri ya Kliniki ya mama na mtoto.

"Tunahitimisha mradi huu kwa mafanikio makubwa tunaomba wanaobaki wasirudi nyuma wazidi kusonga mbele,"alisema Chalamila.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halamashauri ya Wilaya ya Bahi, Zainabu Mlawa, aliishukuru World Vision Tanzania kutokana na kutekeleza mradi huo kwa mafanikio makubwa.

Alisema wakazi wa Mundemu na vitongoji vyake wanapaswa kuendeleza yale yaliyoachwa na World Vision ili waweze kupiga hatua kwenye sekta ya Mama na Mtoto.

Alisema World Vision kupitia wahudumu wao wa ngazi ya Jamii, wamesaidia kwa kiasi kikubwa kuhimiza akinamama waende Kliniki kwa ajili ya kupima afya zao.

Mlawa alisema wataendelea kusimamia suala la afya ya Mama na Mtoto ili kutokomeza kabisa vifo kama walivyofanya World Vision.

Naye Mkurugenzi wa Miradi wa shirika hilo, Simon Moikan, alisema mradi wa AP Mundemu umefanikiwa kwa kiasi kikubwa na kuleta matokeo chanya.

Alisema World Vision iko pamoja na wakazi wa eneo hilo kuhakikisha yale mazuri yaliyoachwa na Shirika hilo yanaendelezwa kimamilifu katika maeneo ambayo mradi ulikuwa unatekelezwa.

# Mahakama yatupilia mbali pingamizi la mawakili kesi ya ulawiti na ubakaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dodoma, imetupilia mbali pingamizi la wakili Leonard Mashabara dhidi ya mawakili wanaowatetea washtakiwa wa kesi ya ulawiti na ubakaji kwa makundi ya kumwingilia kinyume cha maumbile binti wa Yombo Dovya, Dar es Saalam.

Watuhumiwa hao ni pamoja na askari wa JWTZ MT140105 Clinton Damasi maarufu Nyundo,askari magereza C.1693 Praygod Mushi,Load Lema na Nickson Jackson.

Katika shauri hilo Mashabara aliiomba mahakama kuu ya Tanzania kupitia uhalali wa uwakilishi wa washtakiwa katika kesi ya jinai namba 23476 ya mwaka 2024 inayowakabili vijana wanne wanaokabiliwa na kesi hiyo.

Shauri hilo lililetwa mahakamani Agosti 23, 2024 mbele ya Jaji Suleiman Hassan. Wajibu maombi kwenye shauri hilo walikuwa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG). Mawakili wanaowawakilisha washtakiwa ambao ni wanne na washtakiwa wenyewe pia ni wanne.

Akitoa uamuzi mdogo juzi, Jaji Hassan amesema mmoja wa wajibu maombi ambaye anawatetea mawakili wanaowawakilisha akina Nyundo na wenzake alileta mapingamizi sita ya awali kuhusu uhalali wa kufunguliwa shauri hilo.

Alisema mapingamizi mawili yaliondolewa na kubaki manne ambayo ndiyo yaliyowasilishwa mbele ya Mahakama Kuu na kuungwa mkono na wajibu maombi wengine.

Alisema kati ya mapingamizi hayo manne yaliyoletwa mahakamani, ni pingamizi moja ambalo limesema baadhi ya wajibu maombi hawahusiki kwenye kesi ya msingi iliyoko kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma.

Aliwataja wajibu maombi hao kuwa ni TLS, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mawakili wanaowatetea Nyundo na wenzake ambao wapo wanne.

Alisema wajibu maombi hao hawawezi kujibu maombi kwenye shauri lililofunguliwa mahakama kuu kwa sababu hawahusiki kwenye kesi ya msingi iliyoko kwenye mahakama ya chini.

"Hivyo katika shauri hili mleta maombi (Leonard Mashabara) alishirikisha watu ambao siyo sehemu ya kesi ya msingi iliyoko mahakama ya hakimu mkazi Dodoma jambo ambalo ni kinyume cha sheria. Uamuzi wa mahakama ni kwamba maombi hayo hayako sawa kisheria na mahakama inayatupilia mbali," alisema Jaji Hassan.

Katika shauri hilo, wajibu maombi walikuwa 11 ambapo wa kwanza hadi wa saba waliwakilishwa na wanasheria wao huku wajibu maombi wa nane hadi wa 11 ambao ndiyo washtakiwa katika kesi ya kubaka kwa kikundi na kumwingilia kinyume na maumbile binti wa Yombo Dovya Jijini Dar es salaam walijitetea wao wenyewe (hawakuwa na wakili).

Akizungumza nje ya mahakama, wakili anayewawakilisha mawakili wanaowawakilisha kina Nyundo, Robert Owino, alisema baada ya Mahakama Kuu kutupilia mbali maombi hayo, kesi ya kina Nyundo itaendelea kusikilizwa kama ilivyopangwa kama waleta maombi hawatakata rufani.

Naye wakili anayemtetea Mashabara, Emmanuel Anthony, alisema wakati wanafungua shauri hilo, walikuwa wamewajumlisha watu wengine ambao walidhani walikuwa ni mahusus kusikilizwa lakini mahakama kuu imeona kuwa watu wale hawakupaswa kujumlishwa kwenye shauri lile.

Alisema kwa msingi huo shauri walilokuwa wamelifungua limeondolewa na wamepokea uamuzi huo ambao hauathiri maamuzi ya mteja wake.

"Kwa hiyo maelekezo aliyo nayo (Mashabara) ni kwamba nikarekebishe yale maombi na tuyarudishe mahakamani kitu ambacho tumeshakifanya kwa hiyo tunategemea kuanzia labda kesho (jana) tunaweza kuwa na majibu ya nini tutakachokifanya kutokana na hayo maombi yetu hapa hapa Mahakama Kuu," alisema Anthony.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kushoto), akijadiliana jambo na Mbunge wa jimbo la Makete, Festo Sanga, bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CHAVITA yahamasisha uchaguzi wa mitaa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Mkoa wa Dodoma, kimewataka wanachama wenye ulemavu wa kutosikia kujiamini na kujitokeza kugombea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa unatarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu.

Mwenyekiti wa CHAVITA, Mkoa wa Dodoma, Yusuph Mloli, alisema hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za chama hicho kwa kipindi cha mwaka 2022 /23 kwenye kikao kilichowakutanisha viongozi kutoka wilaya za mkoa huo.

Mloli alisema watu wenye ulemavu huo ambao wana vigezo na sifa ya kuwa viongozi kwenye nafasi za uwenyekiti wa serikali za mitaa na vijiji, wajiamini na kujitokeza na kuacha hofu inayowafanya kujinyanyapaa wenyewe kwa kuhofia kutochaguliwa.

Alisema pamoja na kujitokeza kugombea nafasi hizo pia wanapaswa kujiandikisha kwenye uboreshaji wa daftari la kudumu la mpiga kura.

"Hii ni pamoja na siku ya kupiga kura ili kuwachagua viongozi wanaowataka wataofanya kazi zao kwa uzalendo zaidi badala ya ubinfsi," alisema.

Kuhusu utekelezaji wa shughuli za chama, aliwataka wanachama kutoongopa kuwawajibisha viongozi wao wanaokwenda kinyume na kanuni na kuwagawa.

"Ninawaagiza wanachama wetu wa CHAVITA mkoa wa Dodoma, muache kuwaogopa hawa viongozi ambao mtakaowaona utendeji wao ni mbovu wanataka kuwagawa kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa ,badala ya kuwaunganisha kuwa kitu kimoja kwenye chama chetu"alisema.

Naye Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, Justini Ng'wantalima, aliwataka viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu kuwahamasisha wanachama wao kushirikiana na serikali ili waweze kujitokeza kujiandikisha na kupiga kura kuchagua viongozi watakao wasaidia kutatua changamoto zao.

Aidha, aliwataka wanachama hao kutumia nafasi hiyo ya uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji kwenda kuwachagua watakaokuwa na uwezo wa kutatua kero zinazowakabili watu wenye ulemavu katika kufikia malengo yao.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Jiji la Dodoma, Rachel Balisinja, akizungumza kwenye kikao hicho, aliwaomba viongozi wa ChAVITA kuwahamasisha wanachama wake ili kushiriki kikamilifu kwenye mikutano ya kampeni ya vyama vya siasa.

Alisema mikutano hiyo ni muhimu kwao kwa kuwa ndiyo itakayowapa nafasi ya kuwatambua viongozi ambao watakao saidiana na serikali katika kutatua changamoto walizonazo.

Hata hivyo, aliwataka kutofanya makosa ambayo yatakayo wafanya kujutia uamuzi wao wa kuchagua viongozi wasiyo na sifa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.



# Waziri ataka ugawaji majongoo bahari kuwafikia wahusika pekee

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaaban Ali Othman, amewaagiza wasimamizi wa ugawaji wa vifaranga vya majongoo bahari kuwafikia walengwa waliokusudiwa ili kufikia malengo ya uzalishaji.

Waziri Shaaban alitoa agizo hilo jana wakati wa ugawaji wa vifaranga 12,000 vya majongoo bahari kutoka kampuni ya uzalishaji wa mazao ya baharini ya Marine Hatchery kwa vikundi sita vya ufugaji wa mazao hayo katika bahari ya Unguja.

Alisema serikali imelenga kuvigawa bure vifaranga hivyo kwa wafugaji wadogo na si wafanyabiashara, hivyo ni vyema wahakikishe hawapewi wafanyabiashara.

Waziri Shaaban pia aliagiza wataalamu wa wizara kupitia kampuni ya Marine Hatchery kuhakikisha wanaokabidhiwa vifaranga hivyo, wanapata elimu ya kuvitunza na kuvilea pamoja na kuyatembelea mashamba yao kila baada ya wiki mbili ili kubaini changamoto ya ukuaji wa vifaranga.

Alisema kulea vifaranga vya majongoo bahari kunahitaji umakini mkubwa, hivyo serikali itahakikisha inayaboresha mashamba ya wafugaji waliopatiwa vifaranga hivyo pamoja na kuwapa nyavu bure ili kukidhi vigezo vya ufugaji.


Kuhusu masoko, Waziri Shaaban alisema serikali itahakikisha inatengeneza mifumo mizuri ya kununua matango bahari kwa bei ya juu kwa wafugaji waliokabidhiwa vifaranga hivyo ili wanufaike na ufugaji huo.

Pia aliwataka wazalishaji wa vifaranga hivyo kuongeza kasi ya uzalishaji ili kufikia azma ya serikali ya kugawa vifaranga laki moja kwa wafugaji wa matango bahari. Mkurugenzi Mtendaji wa Marine Hatchery, Sheha Idrissa Hamdan, alisema kampuni hiyo kwa kipindi kifupi imezalisha vifaranga milioni 1.1 ambavyo vinatosheleza kwa mashamba yote ambayo yako Zanzibar na maeneo jirani.

Alisema ugawaji wa vifaranga 12,000 vilivyotolewa kwa vikundi sita vya Unguja utakuwa endelevu kwa kuwa Oktoba, mwaka huu, vitagawiwa vifaranga vingine 30,000. Pia alisema Disemba vitatolewa vifaranga vingine 30,000 kwa wafugaji ili kuondosha uhaba wa vifaranga.

Mkuu wa Uzalishaji wa Marine Hatchery, Feisal Shahbai, alisema upatikanaji wa vifaranga ya majongoo bahari ni gharama na iwapo vilivyogawiwa kwa wafugaji vingeuzwa vingegharimu Sh. milioni 90, hivyo ni vyema wafugaji wakaona umuhimu wa kuvitunza ili kuinua hali zao za maisha na kukuza uchumi wa nchi.

Alisema kampuni itahakikisha inawapa elimu wafugaji na kuyatembelea mashamba hayo ili kufikia adhima ya kuanzishwa kwa uchumi wa buluu Zanzibar



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga akizungumza wakati wa uzinduzi wa jukwaa la wakuu wa taasisi binafsi, Mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makandarasi bora kupewa kazi ujenzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema serikali itaendelea kufanya kazi na makandarasi waliofanya vizuri katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya maendeleo.

Pia amewataka makandarasi wazalendo kuendelea kujitolea kuijenga nchi kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa ukarabati wa miundombinu ya elimu ikiwamo shule zilizochakaa, hafla iliyofanyika Cheju, mkoa wa Kusini Unguja.

Hemed alisema azma ya serikali ni kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora bila ya malipo na wanaingia shule katika mkondo mmoja.

Alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga shule mpya za ghorofa na kuzikarabati shule za zamani ambazo zimeshachakaa.

Ali Masoud Naibu, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kusini Unguja, alisema uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya elimu unalengo la kuimarisha ubora wa elimu kwa kuongeza madarasa na wanafunzi kupata elimu bora katika mazingira mazuri.

Alisema serikali itajenga madarasa 2,037 na ujenzi huo utafikia madarasa 4,310 katika serikali ya awamu ya nane Zanzibar sawa na asilimia 237 ya utekelezaji wa ilani ya CCM.

Alisema mradi huo wa miundombinu ya elimu utagharimu shilingi Bilioni 384.8 na utasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa, alisema serikali inatoa elimu bila ya malipo na ndani ya miaka mitatu imeshawekeza Sh. bilioni 800 katika elimu.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alisema mkoa unatarajia kupata majengo matatu ya ghorofa ya shule pamoja na ujenzi wa mabweni ya wanafunzi ili kujenga mazingira bora ya elimu.

# Wananchi walia na ubovu wa barabara

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa vijiji vya Ole Simaongwe, Shumindu na Makaani katika Shehia ya Mjiniole, Chake Chake kisiwani Pemba, wameiomba serikali kuwatengenezea barabara zao ambazo zimekuwa kikwazo kikubwa katika shughuli zao hasa kipindi cha mvua.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi wa maeneo hayo walisema barabara hizo ni muhimu kwa wananchi na wafanyabiashara ambao ni sehemu ya kukuza uchumi wao na kuongeza pato la taifa.

Walisema wanahitaji kuangaliwa kwa jicho la huruma kutokana na uchakavu wa barabara hizo ambazo ni shida kupitika hasa wakati wa mvua na zinahitaji kuwekewa madaraja.

Kwa mujibu wa wananchi hao, ikiwa zitaendelea kupaki hivyo, zinaweza kuhatarisha maisha ya watu wakiwamo watoto ambao wanakwenda shuleni na madrasa na kinamama wanaofanya shughuli za kilimo.

Mmoja wa wananchi hao, Fatma Ali Hamad, alisema barabara hiyo ni ya muda mrefu ambayo walitumia tangu babu zao ingawa hali yake kwa sasa haridhishi kutokana na ubovu.

"Barabara hii ni kongwe ambayo inatoka Kangagani mpaka Dodeani. Ilikuwa ikirahisisha safari za watu wanaokwenda hospitali ya vitongoji lakini sasa hivi mpaka uzunguke Kianga. Kwa kweli tunapata shida sana," alisema. Naye Bimkubwa Hamad Juma alisema katika barabara hiyo kuna sehemu ya daraja iliyoharibika, hivyo wakati wa mvua hapapitiki na wanaosumbuka zaidi ni wanawake na watoto ambao hawawezi kuvuka.


Mwananchi mwingine, Hamad Khatib Hamad, alisema pia barabara inakwenda mpaka Kwareni inahitaji kutengenezwa kwa sababu inachangia ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa, hivyo kuna haja ya kufikiriwa na kujengwa kwa haraka.

"Matofali, mawe, kokoto na kifusi kinachotengenezewa barabara vinakuja kuchukuliwa huku Makaani Kwareni. Pia kuna wakulima wengi wa mboga lakini cha kushangaza barabara hiyo haijatengenezwa na inapofika kipindi cha mvua balaa huwa zaidi kwa sababu haipitiki na wakati mwingine magari yanakwama," alisema.

Sheha wa Shehia hiyo, Hamad Said Mgau, alisema tayari wameshafikisha taarifa katika ofisi ya mkuu wa wilaya ingawa mpaka sasa hazijatengenezwa.

Alisema barabara hizo ni kiungo muhimu na kikubwa cha kuimarisha uchumi wa wananchi na Serikali, hivyo ni vyema zikafikiriwa na kuingizwa kwenye orodha ya utengenezaji wa barabara za ndani.

Afisa Mdhamini Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Ibrahim Saleh Juma, alisema serikali inaendelea na mpango wake wa kujenga barabara za ndani ambapo kwa sasa wanaendelea na ujenzi wa barabara 134, hivyo zitakapomalizika wataendelea na zingine.



**CHINO**
UKURASA 12





# SAWA UNAYE
# Lakini ukimzingua....

MWANAMUZIKI na Mjasiriamali, Shilole, ameonekana kuwaumiza moyo wanaume alioachana nao kwa kueleza kwamba anachopewa na mpenzi wake mpya hajawahi kupata katika maisha yake yote.

Hivi karibuni Shilole, amemtambulisha mpenzi wake mpya huku akieleza kwamba tofauti na wanaume wake wa mwanzo walikuwa wakiishi nyumbani kwake, huyu wa sasa amehamia kwake.

Amesema maisha ya kukaa kwa mwanaume kuna raha nyingi, na kumfanya ajione kama amezaliwa upya.

Kauli hiyo, imewaibua wadau wa muziki na kueleza kwamba kama anachozungumza kinatoka moyoni basi wanatarajia kutoachana na badala yake wataishi kwa muda mrefu.

Shukuru Saidi, amesema Shilole ni mwanamke mwenye msimamo mkali linapokuja suala la mapenzi, kitendo cha kukubali kuhamia kwa mwanaume inaonesha ni jinsi gani ameamua kubadilika.

"Tumemzoea Shilole mwenye tabia ya kubadilisha wanaume kila mara, lakini kwa huyu wa sasa tunaona mabadiliko hasa kuhamia kwa mwanaume ni jambo ambalo wengi hatukulitarajia," amesema Saidi.

Hata hivyo, amemshauri mwanaume huyo kuwa makini na Shilole kwa sababu ni mwanamke anayejiamini na asiyetaka kuumizwa.

"Shilole ana fedha, mapenzi kwake ni suala la kimaumbile tu na sio kusaka maisha, hivyo mwanaume anayekuwa naye ni lazima kujitambua kwani utakapokwenda kinyume na misimamo yake kuvunjika mapenzi sio jambo la ajabu kwake," ameongeza.

Aidha, amemtaka mwanamuziki huyo kutulia na mwanaume mmoja kwa muda mrefu kwa sababu umaarufu na mafanikio yake yamewafanya vijana wengi kumuona kama mtu wa mfano katika kutafuta maisha.

BASI SAWA

## Chino humwambii kitu kwa Nature



MKALI wa muziki wa Amapiano, Chino, amemuelezea mwanamuziki mkongwe wa Bongo Fleva, Juma Nature, kama nyota isiyofifia na kila mtu anapenda kufanya naye kazi.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Chino, amesema kwamba alipokuwa mdogo alikuwa na mapenzi na msanii huyo kutokana na tabia yake ya kuwa karibu na kila mtu.

"Nikawa namuomba Mungu anipe uhai niweze kumuona siku moja kutokana na kuvutiwa na maisha yake. Niliweza kumuona na kuwa rafiki yangu mkubwa tangu nikiwa dansa natamani nifanye nae jambo moja ikiwa kama zawadi na shukrani juu yake kwa mafunzo mema aliyofanya na kuyaacha kwa kipindi chake chote," ameandika Chino.

## Rayvanny alia kuhujumiwa TMA



MSANII maarufu wa Bongo Fleva, Rayvanny, ameonekana kutokubaliana na kinachoendelea katika tuzo za wanamuziki bora Tanzania (TMA), akisema hawezi kuhimili fitna anazofanyiwa.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, mwanamuziki huyo ameomba Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) ambalo linasimamia tuzo hizo kuondoa jina lake kutokana na baadhi ya watu wachache kufanya mambo yasiyofaa dhidi yake.

"Binafsi napongeza serikali yangu kwa jitihada nzuri za kukuza na kuinua sanaa yetu, naunga mkono asilimia mia Wizara na baraza kuandaa tuzo. Hata hivyo sikubaliani na fitna za watu wachache, hivyo kwa unyenyekevu mkubwa ningeomba kuondolewa au kutolewa  kwenye tuzo zetu," amesema Rayvanny.



# MARIOO SASA KANYAGA MWENDO

MWANAMUZIKI Marioo, amejiunga na orodha ya wasanii wanaomiliki lebo ya muziki, na kuleta ushindani mkali katika tasnia ya muziki.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Marioo ameweka wazi kwamba lebo yake ya Bad Nation, itakuwa ya moto na hivi karibuni itamtambulisha msanii wake wa kwanza.

Marioo sasa atashindana na wanamuziki wengine maarufu wanaomiliki lebo kama Diamond Platnumz (WCB ina wasanii watano}, Ali Kiba (Kings Music yenye wasanii watano, Rayvanny (Next Level wasanii wawili, Harmonize (Konde Gang wasanii wawili na Nandy (The Afrika Princes) yenye wasanii wawili.



# Akothee asimulia maisha kitabuni

MWANAMUZIKI na mjasiriamali kutoka Kenya, Esther Akoth, maarufu kama Akothee ameonesha kwa mara ya kwanza mwonekano wa kitabu chake ambacho kimebeba machungu na furaha aliyopitia kwenye maisha yake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Akothee alichapisha  kitabu hicho chenye jina la 'Turn your pain into purpose' na kuelezea kuwa, wasomaji watajua maisha yake halisi na  mihangaiko katika kutafuta mafanikio ya kimuziki, mapenzi na elimu.

"Ni maumivu gani ambayo huwezi kuyasahau na unajihisi kulia kuhusu mambo ambayo unafikiri huwezi kubadilisha, kwa nini unayabeba kila mahali? Je, tunaweza kutembea pamoja kupita maumivu yako? Amehoji Akothee katika ujumbe aliowatumia mashabiki wake.

FILAMU

# Azuka:Mfalme kaumbuka

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI ni dhamama, mtu anapoupata anatakiwa atumikie wananchi na si wananchi wamtumikie yeye. Kuna watu ambao wakipata mamlaka wanayatumia si tu kwa manufaa yao, bali hata kufanya mambo ambayo ni kinyume na maadili. Wapo ambao wakipata uongozi, basi si tu huwa wala rushwa na kujilimbikizia mali, lakini pia kujihalalishia mpaka kuchukua wanawake ambao si wa kwao.

Mtunzi wa filamu ya 'Azuka' ameona mbali sana kuandika hadithi hii ambayo itakuwa ni fundisho kwa watu waliopewa dhamana, wasivuke mipaka yao kwa sababu wanajua watalindwa na dola kutokana na uongozi wao. Ipo siku uongozi unakwisha na yote hayo yanalipwa.

Imechezwa na baadhi ya waigizaji ambao ni Mwadua Jawa ambaye ni mtunzi na akacheza kama mfalme, Hussein Al Eda na Hassan Al Eda, Bi Jasi, Salima Lema, Kibeku, Fatime Abdallah aliyecheza kama Azuka.

Kwenye himaya ya mfalme Kaiwanga, kuna binti mmoja mzuri ambaye ndiyo anaingia sasa kwenye usichana wake, Azuka. Ubichi na urembo wake unamzuzua mpaka mfalme. Anaamua kuwaambia walinzi wake wakamchukue na kumletea kule porini walikoenda. Anambaka na baada ya kumaliza kumuonya kama akitoa siri hiyo, basi atauawa.

Siku ya ngoma kwenye himaya Vunde inafika, wasichana wote wanatakiwa kwenda kucheza ngoma. Azuka anashindwa kucheza, japo ni msichana mdogo, na cha ajabu zaidi akaanza kutapika. Uchunguzi ukaonesha kuwa ni mjamzito. Habari ikamfikia mfalme na kuamua akamatwe kwa siri na kutupwa kwenye msitu mnene akaliwe na wanyama. Walinzi wanatekeleza. Waliporudi kumpa habari kijana mmoja aitwaye Dovisa anasikia siri hiyo. Wanamshtukia, na yeye akamatwa na kwenda kumtupa kwenye msitu huo.

Mizimu inawalinda Dovisa na Azuka kwa sababu hawana hatia. Mzimu unawatokea msituni na kuwaagiza kwenda kwenye himaya kueleza ukweli wote.

Ngoma inawaita wanahimaya wote bila mfalme kuwa na taarifa. Wakati mke wa mfalme anashangaa, Azuka na Dovisa wanatokea na kueleza ukweli wote. Mzimu wa msituni uliowalinda nao utajitokeza kuja kushindilia na kukazia hoja. Unawaadhibu walinzi, na mfalme mwenyewe kwa kuwaangamiza. Azuka mwenye ujauzito wa mfalme na Dovisa wakaushikilia utawala wa mpito.




# PENZI LIKIISHA NI SUMU

**Na Adam Fungamwango**

PENZI ni kitu cha ajabu sana duniani. Linampa binadamu furaha, amani, utulivu na kila aina ya faraja.

Penzi linapoanza na kuwa kileleni ndiyo wakati ambao hakuna yeyote anayeona mapungufu au kasoro yoyote ya mwili na tabia. Kwenye pengo huona kuna mwanya na kwenye chongo huona kuna kengeza.

Mwenye kupenda haoni wala hasikii. Penzi ni dawa.

Kwa bahati mbaya likianza kuchuja ndipo hapo linapokuwa sumu. Kuna watu dunia wanaiona chungu. Wanaona hata dunia yenyewe si sehemu salama ya kuishi. Baadhi wanaishia kujinyonga. Na hata ambao hawafanyi hivyo wanachukua muda mrefu hadi kurejea kwenye hali ya kawaida, inategemea na kichwa cha mtu mwenyewe. Hiyo ni baada ya 'kupigwa chini' au kuamua kuacha mwenyewe kwa sababu mbalimbali, kuu ni kutendwa.

Hapa leo tunaangalia nyimbo za dansi ambazo zinaonesha penzi linapokuwa limefikia ukingoni, liwe la mke na mume, au hata wapenzi.

### Solemba-Juwata Jazz Band

Huu ni wimbo wa Juwata Jazz Band uliorekodiwa mwaka 1985, ukitungwa kuimbwa na mwanamuziki mlemavu wa macho, Nico Zengekala aliyefariki miaka miwili baada ya kutoa wimbo huo 'Solemba'.

Unamzungumzia mtu mmoja ambaye ameamua mwenyewe kulivua penzi, baada ya mwanamama aliyempenda kuonyesha kuwa hana habari naye.

Jamaa alienda nyumbani kwa 'demu', lakini badala ya kukaribishwa 'akachomeshwa mahindi', kuanzia asubuhi hadi saa nane jua likimuunguza.

Akarudi nyumbani kwa kuamua kuwa liwalo na lile penzi basi.

### Tereza-Vijana Jazz Band

Huyu jamaa ndiyo anatia huruma kabisa. Huyu akakataliwa siku ya harusi mbele ya kasisi na jamaa na marafiki waliofika kwenye sherehe hizo. Hebu pata picha aibu yake ikoje?

Mwanamama anaitwa 'Tereza'. Alikuwa mpenzi wake na akakubali kabisa kuolewa. Alichokifanya siku ya harusi kimebaki kuwa historia.

Wimbo ulitungwa na kuimbwa na Jerry Nashon mwaka 1990, akiwa na Vijana Jazz Band.

### Edita-DDC Mlimani Park

Kuna vitu vingine vya kusikitisha sana. Kwenye wimbo huu, jamaa anamlalamikia mpenzi wake anayeishi naye nyumba moja, kumsaliti na kumletea mwanaume ndani ya nyumba yake.

Jamaa kila siku anaambiwa kuwa mpenzi wako si mwaminifu, lakini alijua ni fitina tu za majirani. Kila anaporudi kazini hamkuti, akimuliza anaambiwa alikwenda kwa shangazi yake kariakoo, kumbe yupo na bwana. Siku alipomfuma ndani ndiyo yalipomshinda, akanawa maji.

Umetungwa na kuimbwa na Hasaan Rehani Bitchuka akiwa na DDC Mlimani Park, katikati ya miaka ya 1980.

### Makumbele-Maquiz Original

'Makumbele' ni wimbo wa miaka ya mwanzoni mwa 1990, utunzi wake mpiga 'trumpet' Kaumba Kalemba.

Unamzungumzia, mama mmoja anayemlalamikia mume wake ambaye amemfanyia mambo mengi mabaya, lakini sasa imetosha, amefika mwisho anarudi kwa baba na mama yake.

### Siwema-Dar International

Wimbo huu wa miaka ya 1980, ulitungwa na Marijani Rajab akiwa na bendi ya Dar International. Unazungumzia jamaa mmoja akimlalamika mpenzi wake Siwema ambaye kumpenda kwake kukafanya kumtangazia kuwa amemuweka kwenye kiganja.

Jamaa kashtuka, kaanza kumwambia kuwa yeye hababaiki na sura, anapenda tabia njema tu.



# Solidstar anajua kumlinda

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Solidstar amewajibu watu wale wanaomsema vibaya mke wake kupitia mitandao ya kijamii.

Katika chapisho lake kwenye ukurasa wa Instagram, Solidstar alitumia maneno makali akiwataka watu hao waache kumdhihaki mkewe kwani mapitio yake ikiwa mazuri au mabaya ni jambo analolithamini.

Wafuasi wake wamekuwa wakimshauri mwanamke huyo kuachana naye wakidai mwanamuziki huyo amekithiri vitendo vya unyanyasaji.




## TG Omori ajipa matumaini

BAADA ya kushindwa kupandikizwa figo, mwongozaji maarufu wa video za muziki, TG Omori, amewahakikishia mashabiki wake kuwa atakuwa sawa hivi karibuni.

Omori ametumia ukurasa wake wa Instagram, kuweka picha yake akiwa hospitalini akiwa na barakoa ya oksijeni, na kuwataka mashabiki wake kutokuwa na huzuni.


"Nitakuwa vizuri hivi karibuni, nawaahidi" amewaambia mashabiki wake na kufuatia jumbe nyingi za kumtakia kupata nafuu ya haraka.

## Krane kapata alichokitaka

SAKATA la wanamuziki wa Nigeria, Dammy Krane na Davido limechukua sura mpya, baada ya polisi kumkamata na kumwachilia Krane kwa tuhuma ya kutoa kashfa.

Katika video hiliyosambaa mitandaoni inamuonyesha Krane akitoa shukurani kwa mashabiki zake baada ya kuachiliwa na polisi.

Davido alifungua mashtaka polisi kutokana na Krane hivi karibuni kueleza kuwa msanii mwenzake huyo alitoa pesa ili afunguliwe kesi ya utakatishaji wa fedha.





## Peter Okoye hataki upotoshaji

WAKATI mzozo ukiendelea kati ya wanamuziki maarufu ambao ni ngucu, Paul na Peter Okoye, yawezekana hali inaweza kutulia na wawili hao kurudi tena pamoja.

Matumaini hayo yamekuja baada ya Paul Okoye, maarufu kama Rudeboy, sasa amekataa kuzungumzia ugomvi wao kutokana na upotoshaji unaofanywa na baadhi ya watu.


'Nitasema kitu, nimechoshwa na upotoshaji huu wa kauli; wewe ni shabiki wa Psquare na ni familia yangu. Kwa hivyo kwa nini niseme kitu sasa ambacho kingegeuka kuwa kitu kingine? Wacha tushikamane na Rudeboy," alimwambia mwandishi mmoja aliyetaka ufafanuzi kuhusu mgogoro huo.

## Olorungbebe afariki dunia

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, Yusuf Olorungbebe amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Taarifa ya kifo cha mwigizaji huyo zilitangazwa na msanii mwenzake Foluke Daramola, kupitia ukurasa wake wa Instagram na kueleza alifariki siku chache baada ya video yake akionekanamelazwa hospitalini kusambaa mitandaoni.

"Tumempoteza Yusuf Olorungbebem tunajisalimisha kwa Mapenzi ya Mungu. Asanteni Wote!" ameandika Daramola.







## Wamlilia Aweso kwa ukosefu wa maji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wa Kijiji cha Korini Kusini katika Kata ya Mbokomu, Moshi mkoani Kilimanjaro, wanakabiliwa na uhaba wa maji kwa zaidi ya miezi minne.

Hatua hiyo imesababisha wananchi hao kununua maji lita 20 kwa Sh. 500 na kusafirisha kwa usafiri wa pikipiki Sh. 1,500.

Wakizungumza na Nipashe kwenye mkutano wa hadhara wa kijiji ambao uliahirishwa kwa amri kutoka juu, mmoja wa wananchi hao, Musa Kyara, alisema kwa sasa wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji na kumwomba Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kuingilia kati.

Alisema wanalazimika kuchukua maji katika Kijiji cha Tera au kusubiri gari linalouza maji ndoo moja Sh. 500 na ili kutimiza mahitaji ya nyumbani. Walisema mahitaji kwa siku ni takriban ndoo sita ambazo kwa kununua wanahitaji Sh. 3,000

"Mume wangu ananiachia pesa ya matumizi 5,000 nanunua maji ya 3000, nabakiwa na Sh. 2000 haitoshi kula familia ya watu watano. Mwisho wa siku tunaishia kugombana kuwa nina matumizi mabaya ya pesa,

"Tunalazimika kulipa kutokana na umbali wa kufuata maji hayo ni zaidi ya kilomita tatu ijapokuwa si safi na salama. Magonjwa kama UTI kwetu yameweka kambi. Tunaiomba serikali kuangalia kwa kina," alisema Trifonia Mrema

Naye Justina Urio alisema bado kuna suala la wanafunzi wako hatarini kupata ugonjwa ya kipindupindu kutokana na kukosekana kwa maji na vyoo vyao kuwa vya kisasa, hivyo vinavyohitaji maji mengi.

"Wako walio katika umri wa kubalehe, wanapoingia kwenye siku zao bado ni tatizo kubwa." Alisema.

Mkazi mwingine, Futunatus Ndiyerimo, alisema sababu kubwa ya tatizo hilo ni chanzo cha maji kosombwa na mafuriko nyakati za Eli-Nino jambo ambalo serikali bado imekaa kimya hadi sasa.

# Upungufu damu chanzo ukuaji hafifu mtoto

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

UPUNGUFU wa damu mwilini kwa wajamzito umetajwa kuwa chanzo cha ukuaji hafifu wa mtoto tumboni, kuzaliwa na uzito pungufu, na hatimaye kushindwa kufanya vizuri darasani anapoanza masomo.

Daktari kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Ludovick Legama, alisema hayo jana wakati wa mahojiano maalumu na Nipashe kuhusu athari za upungufu wa damu kwa mjamzito na mtoto tumboni.

Dk. Legama alisema mjamzito akiwa na upungufu wa damu mtoto ukuaji wake utakuwa hafifu, uzito wa mtoto utakuwa chini ya kilogramu 2.5.

Pia, alisema ukuaji wa akili wa mtoto utaathirika ambapo akianza shule darasani anaweza asifanye vizuri mama yake kama alikuwa na upungufu wa damu kwa kipindi kirefu.

Dk. Legama alisema kuwa mama akiwa na upungufu wa damu kwa muda mrefu anasababisha utengenezwaji wa ubongo kutokwenda vizuri na kumsababishia madhara mtoto akizaliwa.

"Kipindi mama akiwa mjamzito upungufu wa damu unaangaliwa umri wa ujauzito na ndani ya miezi mitatu upungufu wa damu ukiwa chini ya gramu 11," alisema Dk. Legama.

Mtaalamu huyo wa afya alisema ndani ya miezi minne mpaka tisa upungufu wa damu ukiwa chini ya gramu 10.5 kwa desimita ya damu mama anakuwa na upungufu wa damu.

Alitaja chanzo cha upungufu wa damu kwa mjamzito kuwa ni upungufu wa virutubishi vinavyotumika kutengeneza damu kama vile madini chuma na vitamini B12 na B9.

Alitaja vyanzo vingine kuwa ni uwepo wa baadhi ya magonjwa kama malaria ambayo inashambulia sana damu hasa seli nyekundu, ugonjwa wa minyoo, ugonjwa wa figo na ugonjwa wa ini.

Vilevile, alisema vidonge vyenye madini chuma na folic acid vina maudhi ila wasiache kuvitumia kwa sababu ya ladha ya dawa ni lazima kwao.

Alisema licha ya maudhi hayo lakini kuna mjamzito anayeambiwa ameze kidonge kimoja kwa siku na mwingine anaweza kuambiwa ameze vidonge viwili kwa siku ni kulingana na upungufu wa mjamzito alionao.

Naye Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Laurencia Urio, alikiri upungufu wa madini chuma ndio unasababisha upungufu wa damu.

Ofisa huyo alielekeza vyakula vyenye madini chuma ambavyo wajawazito wanatakiwa wavitumie ili kuongeza damu haraka ni nyama, samaki, maini, utumbo, mboga za majani, mashona nguo na choya.

"Vyakula vyanzo vya wanyama ndio vinaongeza haraka wingi wa damu ikiwamo mchicha wa kienyeji, matembele meusi na mashona nguo,"alisema Urio

Alisema ni vizuri mjamzito akawa na damu ya kutosha kabla ya kupata ujauzito.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) dalili za upungufu wa damu mwilini ni kusikia kizunguzungu, kukosa nguvu, kubadirika rangi ya mwili kuwa mweupe kuliko kawaida, kukosa umakini wa kuona vizuri, mapigo ya moyo kwenda mbio.

Dalili zingine ni kushindwa kupumua vizuri na kuvimba miguu lakini madhara yake ni kuwa kwenye hatari ya kupoteza uhai, kuzaliwa mtoto njiti, mtoto kuzaliwa amechoka na ukuaji wa mtoto kuwa wa shida au kudumaa.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita (watatu kushoto), akipokea msaada wa vifaa tiba kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu, katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga juzi, kwa ajili ya kuboresha huduma za afya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu 550 kujengewa uwezo ufundishaji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

HALMASHAURI ya Mji wa Babati mkoani Manyara, imesema imewapatia mafunzo walimu 551 kazini kwa ajili ya kuwaongezea uwezo wa kufundisha wanafunzi kuanzia darasa la awali mpaka darasa la saba.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri hiyo, Simon Mumbee, alisema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu namna wanavyoboresha sekta ya elimu kuanzia darasa la awali ili kuwajengea wanafunzi umahiri wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Alisema mpango huo, unaitwa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) ,ambao ni miongoni mwa maeneo manane yanayofanyiwa kazi na programu ya kuboresha elimu ya msingi (BOOST).

"Tulifanya mafunzo kwa walimu wote kwa asilimia 100 Januari, mwaka huu, walikuwa 551 na walimu hawa ndani yao kuna walimu wa darasa la awali na darasa la kwanza," alisema Mumbee.

Pia, alisema lengo kuu ni wanafunzi wa awali na darasa la kwanza wajue kusoma, kuandika na kuhesabu(KKK).

Alisema kwenye Programu ya BOOST, kuna maeneo manane ya kufanyia kazi ambayo ni uandikishaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza, uboreshaji wa miundombinu, usalama wa watoto yaani shule salama, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), mafunzo endelevu ya walimu kazini, bajeti na utawala bora.

Mumbee alisema katika vipengele hivyo, halmashauri inayofanya vizuri kwenye kipengele kimojawapo, inapata fedha za ziada kwa ajili ya kuboresha huduma za elimu.

Pia, alisema kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 2023 kuanzia darasa la kwanza wanaanza kujifunza somo la Kiingereza ili kuwaongezea maarifa toka wakiwa wadogo.

Kwa mujibu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), haki ya watoto wote ya kupata elimu si tu lengo la nne la ajenda ya 2030, bali imewekwa katika mkataba wa haki za mtoto na mikataba na matamko mengine ya kimataifa ambayo yanahitaji elimu ya msingi iwe bure na lazima kwa wote.

Naye Mshauri wa malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM), Davis Gisuka, kutoka Shirika la Children In c Cossfire (CIC),, alisema program ya BOOST, inalenga zaidi elimu ya awali na inagusa moja kwa moja suala la malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Aliyataja maeneo mengine ya mradi unakogusa kuwa ni kusaidia kupata zana za kujifunzia kwa wanafunzi, kupunguza tatizo la ukosefu wa madarasa ya awali na unatoa mafunzo ya walimu wa awali.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA



# Mitindo ya 'ogelea piga mbizi', Maquiz, 'Chunusi,' OSS ilivyotetemesha mashabiki

**Na Adam Fungamwango**

MOJA ya miaka ya kufurahisha kwenye muziki wa dansi ni ile ambayo Maquiz Original walipoasisi mtindo wa 'Ogelea piga mbizi'. Ilikuwa ni mwaka 1982. Ni baada ya kutoka kwenye mitindo mbalimbali kama vile 'Chakula chakula kambombe', 'Kamanyola bila jasho', na kwa muda mfupi 'Scania LBT'.

Baada ya mitindo hiyo, Maquiz ambayo awali ilikuwa inaitwa Maquiz Du Zaire, licha ya kubadilisha majina ya mtindo, ilibadilisha na jina hilo, ikawa Maquiz Original.

Kwa mujibu wa kiongozi wa zamani wa bendi hiyo, Nguza Mbangu Viking, ni kwamba waliondoa maneno ya 'du Zaire' kutokana na kwamba wakati huo bendi haikuwa na wanamuziki wa Wazaire tu kama awali, bali walianza kuingia hata wanamuziki wa Kitanzania na mataifa mengine hadi raia wa Comoro.

Wakati Juwata Jazz Band na mtindo wao wa Msondo Ngoma wakiwa na upinzani mkali na DDC Mlimani Park Orchestra wana Sikinde Ngoma ya Ukae, kwa bendi za Kizaire wakati huo, sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kulikuwa na upinzani mkali kati ya Maquiz na Orchestra Safari Sound.

Na upinzani rasmi ulianza pale, Kikumbi Mwanza Mpango, King Kiki alipolipa kisogo kundi la Maqiuz du Zaire chini ya mtindo wa 'Kamanyola bila jasho', mwishoni kabisa mwa miaka ya 1990, na kujiunga na Orchestra Safari Sound.

Ikumbukwe Kiki, alijiunga na Maquiz mwaka 1977, alipokwenda kuchulikuwa nchini Zaire baada ya kuonekana kuwa bendi ilihitaji mabadiliko.

Hakuwa mgeni nchini, kwani mwanzoni mwa miaka ya 1970 alikuwa hapa na bendi ya Orchestra Fauvette iliyotoka Zaire na kuingia nchini miaka hiyo. Kiki alikuwa mwimbaji na Freddie Ndala Kasheba alikuwa ni mpiga gita la solo wa bendi hiyo hiyo, wakatoa vibao vilivyopendwa mno si na Watanzania tu, bali Afrika Mashariki na Kati nzima kama 'Jaqueline', 'Fransisca', 'Vivi', 'Nono na Kalimie', 'Zula' na vingine vingi.

Bendi hiyo baada ya kurejea nchini Zaire, wanamuziki hao walikutana na wenzao na bendi ya Maquiz huko Lubumbashi, Kiki aliwaibia siri kuwa kuna soko kubwa la muziki nchini Tanzania. Ndipo Maquiz Du Zaire ilipofanya safari nchini Tanzania na kuweka makazi.

Ilipoona upinzani wa muziki umekuwa mkubwa, ndipo walipomkumbuka mtu aliyewapa siri ya soko la muziki Tanzania, Kiki, wakamleta nchini mwaka huo.

Kwa kiasi kikubwa aliibadilisha mno bendi hiyo na kubuni mtindo wa 'Kamanyola bila jasho'. Ni kipindi ambacho si jina la Kiki tu kujulikana mpaka akapachikwa jina la King, lakini bendi ya Maquiz du Zaire ikapata mashabiki wengi na kuwa kivutio kikubwa. Ikarekodi nyimbo nyingi zilizopendwa kama 'Kasongo', 'Nasema Sina Ndugu', 'Maggie', 'Dora Mtoto wa Dodoma', 'Chrismass' na nyingine nyingi.

Mfanyabiashara matata wakati huo, Huggo Kisima, alimchomoa Kiki Maquiz du Zaire na kumpeleka kwenye bendi yake ndogo iliyoitwa Orchestra Safari Sound. Aliondoka pamoja na wanamuziki kadhaa. Huko akabuni mtindo wa 'Masantula Ngoma ya Mpwita'. Ikawa balaa. Nyimbo za 'Ni kweli', 'Mwaka wa Watoto', 'Haruna Kaka', 'Hangaika', na zingine ziliifanya bendi hiyo kubwa kubwa. Na hapo ndiyo rasmi ilipoingia ushindani na Maquiz.

Hata hivyo, Kiki alimaliza mkataba wake miaka michache tu baadaye na kijiti kikachulikuwa na mwenzake aliyekuwa naye Fauvette, Ndala Kasheba. Wengi hawajui kuwa Kiki na Kaseba waliingia wote OSS ya Masantula, lakini hakukaa, kabla bendi haujarekodi akaelekea nchini Burundi. Mkataba wa Kiki ulipokwisha, Kisima alimleta Kesheba, ambaye yeye kwanza kabisa alikuja gita la nyuzi 12. kwa wakaida gita lina nyuzi sita, lakini yeye akaja na la nyuzi 12. Ikawa ni habari mpya nchini, mashabiki wakalipachika jina la 'kombora'.

wengine wakaliita 'dazani'.

Nyimbo za kwanza kabisa zilikuwa ni 'Bakambi Nkela', 'Ashura', 'Maudhi ya Roho', 'Ntale', 'Mpakamanga', 'Marashi ya Pemba', 'Njiba' na nyingine ambazo ziliitetemesha Maquiz Original ambayo tayari ilikuwa imemrudisha Kiki kundini, safari hii ikitoa nyimbo kama 'Double Double', 'Anjelu' 'Mapenzi ya mashahidi' na zingine, lakini hakukaa sana akaanzisha bendi ya Orchestra King Kiki Double O.

**Bendi hiyo baada ya kurejea nchini Zaire, wanamuziki hao walikutana na wenzao na bendi ya Maquiz huko Lubumbashi, Kiki aliwaibia siri kuwa kuna soko kubwa la muziki nchini Tanzania. Ndipo Maquiz Du Zaire ilipofanya safari nchini Tanzania na kuweka makazi.**

Ndipo Maquiz walipokuja na mtindo ya 'Ogelea Piga Mbizi'.

Kuona hivyo Kasheba akaja na mtindo ya 'Chunusi'. kwenye andishi lao kwenye matangazo magazetini waliandika kabisa kuwa usicheze na bahari kuna chunusi.

Yaani wote wanaoogelea, watakutana na chunusi. Yeye akajiita ndiyo chunusi mwenyewe. Ikawa inachorwa katuni kwenye magazeti jitu refu lililovaa kofia aina ya pama ambalo lipo katikati ya bahari, naji yamemfika kwenye magoti, akiangalia kama kuna mtu baharini.

Hili lilileta upinzani mkubwa wa kimuziki baina yao. Ilisababisha kunyang'anyana mashabiki, na kukawa na upinzani wa maneno kati ya mashabiki wa pande zote mbili kama ule ubishani tunaouona wa Simba na Yanga mitaani.

Baadaye Maquiz wakapata wazo wakaja na neno 'kafara'. Yaani humo kwenye bahari wamefanya kafara, hivyo wanaweza kuendelea kuogelea na kupiga mbizi.

Hata hivyo, wakaona iswe tabu, wakaacha na mtindo huo, wakaja na 'Sanifu', baadaye 'Zambwela' hadi 'Sendema,'. Mwaka 1985, Kasheba naye alimaliza mkataba wake, bendi ikawa chini ya Muhidini Gurumo na mtindo wa 'Ndekule', hapo ndipo upinzani rasmi ya OSS na Maquiz ulipokufa. Kwa sababu hakupiga muziki unaofanana kama mwanzo.

Mwanamuziki Freddie Ndala Kasheba, kiongozi wa Orchestra Safari Sound (OSS), akiwa na gita lake la nyuzi 12, maarufu kama dazani au kombora, kwenye onyesho la wazi lililofanyika mwanzoni mwa miaka ya 1980, viwanja wa Mnazi Mmoja, Dar es Salaam

**Tuma meseji 0716 350534**

# Ndege vita ya Marekani yadunguliwa Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

NDEGE moja ya kivita aina ya F-16 iliyotolewa na Marekani na wanachama wa Nato kwa Ukraine, imedunguliwa na kuua rubani wake.

Chanzo cha kijeshi cha Ukraine kiliambia BBC, kilisema ndege hiyo ilianguka kufuatia msururu wa mashambulizi ya makombora yaliyofanywa na Russia usiku wa Jumatatu, na kusababisha kifo cha rubani, Oleksiy Mes.

Tukio hilo imeelezwa kuwa ni hasara ya kwanza ndege za aina hiyo kutolewa kama msaada nchini Ukraine mapema mwezi huu.

Hata hivyo, hakuna sababu iliyotolewa kuhusu ajali hiyo kama ilitokana na shambulio la moja kwa moja kutoka Russia.

Ukraine ilisema rubani alitungua makombora matatu ya cruise na droni moja katika shambulio kubwa zaidi la anga lililofanywa na Russia.

"Oleksiy aliwaokoa raia wa Ukraine kutoka kwa makombora hatari ya Russia," Jeshi la Wanahewa la Ukraine liliandika katika taarifa yake kwenye mtandao wa kijamii.

"Kwa bahati mbaya, ilimgharimu maisha yake mwenyewe." Iliongeza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo haikubainisha aina ya ndege iliyohusika, lakini chanzo cha kijeshi kiliambia BBC kuwa rubani alikuwa akiendesha F-16.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alithibitisha rasmi Jumanne kwamba ndege za F-16 zinazotengenezwa Marekani zinatumika kutungua ndege zisizo na rubani na makombora ya Russia.

Zelensky wiki hii, aliomba washirika wake kuruhusu kutumia makombora ya masafa marefu kulenga shabaha zaidi hadi Russia.

Alisema hakutakuwa na vizuizi kwa matumizi ya ndege hizo mbali na kuzingatia sheria za kibinadamu, aliuambia mkutano mmoja akiwa Washington.

Wakati huo huo, mawaziri wa ulinzi wa Umoja wa Ulaya wanakutana nchini Ubelgiji kujadili kuharakisha usambazaji wa mifumo ya ulinzi wa anga iliyoahidiwa awali kwa nchi ya Ukraine.

Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, Josep Borrell, alisema hayo wakati akitoa maoni kuhusu taarifa za Waziri wa Mambo ya Nje ya Ukraine, Dmytro Kuleba, ambaye alilalamikia kuhusu uwasilishaji polepole wa risasi na silaha nyingine kwa vikosi vya Ukraine, vilivyoahidiwa na washirika wa Magharibi.

"Ahadi nyingi zimetolewa tangu Juni mwaka huu, hasa katika eneo la ulinzi wa anga. Kwa kuzingatia mashambulizi makubwa ya miji ya Ukraine, ambayo yamekuwa mashambulizi makubwa zaidi dhidi ya raia, ni wazi kwamba lazima tujibu," alisema Borrell.

"Tutaangalia masuala haya yote, sasa tuko katika kutimiza wajibu wetu. Ni wazi, ikiwa Waukraine wana msaada huo, wanaweza kupigana kwa mafanikio," aliongeza.

Alisisitiza kuwa operesheni katika eneo la Kursk ni mfano mzuri wa hili.

"Hii ni hatua ya kimkakati ya kuamua na yenye mafanikio ambayo inaonesha kuwa wako tayari kupigana na kuendelea kupigana wakati wana msaada wa nyenzo ambao unategemewa kutoka kwetu," alisema.

**BBC**



Picha iliyonaswa ikimuonesha mwanajeshi wa Russia akiwa katika eneo la Donetsk juzi. **PICHA: AP**

# Kamala Harris atetea sera zake kubadilika

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, ametetea mabadiliko yake ya sera, na kumpongeza Rais Joe Biden, kwa kuinua uchumi.

Katika mahojiano yake ya kwanza tangu kuwa mgombea wa chama cha Democratic katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Novemba mwaka huu, Harris alisema

utawala wa Biden uliweza kuokoa uchumi baada ya janga Corona na kupunguza uhamiaji haramu katika miezi ya hivi karibuni.

Aliziita sera za Ikulu ya Marekani ni kama mafanikio, akiashiria kupungua kwa gharama za kupata dawa na kiwango cha ukosefu wa ajira.

"Hiyo ni hatua nzuri. Kuna nafasi ya kufanya vizuri zaidi." Alisema Harris.

Makamu huyo wa Rais, alionekana kwenye mahojiano yaliyorekodiwa ya CNN na mgombea mwenza wake, Gavana wa Minnesota Tim Walz.

Ilikuwa ni mara yake ya kwanza kufanya mahojiano ya aina hiyo kama mgombea urais.

Harris alilazimika kutetea rekodi ya uchumi ya serikali ya Marekani, huku mfumuko wa bei na kupanda kwa gharama ya maisha ikiendelea kuumiza vichwa Wamarekani.

Kura za maoni zimependekeza mara kwa mara kwamba wapiga kura wangependelea mgombea wa Republican Donald Trump, kushughulikia suala la uchumi.

Lakini majibizano makali zaidi kati ya Harris na mwandishi wa CNN Dana Bash, yalijikita katika madai kwamba nafasi za sera za mgombeaji huyo wa Demokratic zimebadilika wakati akiwa makamu wa rais na sasa kama mgombea wa urais. **BBC**

## Kagame awafukuza wanajeshi 214

**KIGALI,** RWANDA

Rais wa Rwanda, Paul Kagame, amewafukuza kazi wanajeshi 214 wakiwemo maafisa wakuu wa kijeshi.

Taarifa fupi ya Wizara ya Ulinzi ya Rwanda iliyotolewa jana, iliyowekwa kwenye ukurasa wake rasmi wa X ilisema maofisa waliofutwa jeshini ni pamoja na Meja Jenerali Martin Nzaramba na Kanali Dk. Etienne Uwimana.

"Pia ameidhinisha kufutwa na kubatilishwa kwa askari 195 wa vyeo vingine vya Jeshi la Ulinzi la Rwanda," ilisema taarifa hiyo.

Hakuna sababu iliyotolewa kuchukuliwa kwa hatua hiyo, Hata hivyo, taarifa hiyo ilitangazwa saa chache baada ya Rais Kagame kukutana na maofisa wakuu wa kijeshi, akiwemo Mkuu wa Majeshi Jenerali Mubarakh Muganga.

Tovuti inayounga mkono serikali ya New Times, iliripoti kwamba kiongozi huyo na maofisa wa kijeshi walijadili vipaumbele vya amani na usalama vya Rwanda. **BBC**

## Burundi yaomba msaada kupambana na Mpox

**BUJUMBURA,** BURUNDI

SERIKALI ya Burundi imeomba msaada wa kifedha kutoka jumuiya ya Kimataifa ili kupambana na ugonjwa wa Mpox, baada ya watu 193 kulazwa hospitalini kwa kuambukizwa ugonjwa huo.

Wizara ya afya ya nchi hiyo ilisema inatafuta karibu Dola milioni 1 kwa ajili ya kupambana na maambukizi yanayoongezeka nchini humo.

Wizara ya afya inasema watu 231 wameambukizwa na ugonjwa huo kufikia Agosti tarehe 25, wengine 38 wametibiwa na kuruhusiwa kwenda nyumbani na hakuna aliyepoteza maisha.

Jumla ya wilaya 29 kati ya 49 zimeripoti kesi za maambukizi ya ugonjwa huo.

Wataalam wa afya walisema elimu inapaswa kutolewa kwa watu wanaokutana kwenye maeneo ya umma kama masoko, makanisa na shuleni ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huo.

Ukosefu wa maji safi ya kunawa kwenye maeneo mengi ya jiji la Bujumbura, inaelezwa kuwa sababu ya kuendelea kusambaa kwa ugonjwa huo ambao huambukizwa kwa watu kugusana na watu walioambukizwa. **RFI**




Viongozi na wanafunzi wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kutembelea moja ya karakana za kampuni ya Group Six International, jijini Dar es Salaam juzi, kwaajili ya kujifunza kuhusu usimamizi wa miradi mikubwa ya ujenzi na majengo makubwa ya kibiashara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waandishi wakumbushwa kuzingatia maadili wanaporipoti uchaguzi nchini

**Jenifer Gilla na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba, amewakumbusha waandishi wa habari kuzingatia maadili wanaporipoti matukio ya uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba mwaka huu, na uchaguzi mkuu Oktoba 2025.

Makoba aliyasema hayo jana katika Kongamano la 14 la Jumuiya ya Mawasiliano ya Afrika Mashariki 2024 unaoongozwa na kaulimbiu Afrika na Mijadala ya Ulimwengu kuhusu Vyombo vya Habari na Mawasiliano.

Aliwasihi waandishi wa habari kuendelea kuwa makini, ili kuripoti taarifa za kweli, zisizo na upendeleo kwa umma na kutoa fursa sawa kwa makundi tofauti.

„Jukumu la vyombo vya habari katika kuzingatia ukweli na uadilifu ni muhimu zaidi sasa kuliko wakati mwingine wowote,“ alisema Makoba.

Aidha, aliwakumbusha waandishi hao kutumia kalamu zao kuielimisha jamii juu ya haki na wajibu wao wa kushiriki kikamilifu katika kuchagua viongozi wanaowataka.

„Vyombo vya habari vinapaswa kusaidia umma kufanya maamuzi sahihi na kushiriki kikamilifu katika michakato ya kufanya maamuzi,“ alisema.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari, ili kuweka mifumo mizuri ya kufanya kazi kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi.

Alisema pia serikali inaendelea na program za kuwajengea uwezo waandishi wa habari, ili kuwapa ujuzi unaohitajika kukidhi mahitaji ya mabadiliko ya teknolojia katika sekta hiyo ikiwamo Akili Mnemba (AI).

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Dk. Derius Mukiza, alisema wanahabari ni lazima wawekeze kwenye teknolojia ya mtandao kwasababu ndiko dunia iliko.

Aidha, wameshauri wanahabari kutumia maendeleo ya teknolojia ya mtandao kama fursa ya kupiga hatua kimaendeleo na katika kushughulikia matatizo ya kitaaluma yanayoikabili sekta hiyo ikiwemo kuzuia usambazaji wa taarifa zisizo sahihi.

"Tunachohitaji katika vyombo vetu na shule za habari ni kuwekeza katika teknolojia na ubunifu kwa nguvu zote ili tusiachwe nyuma na wenzetu ambao tayari wamepiga hatua zaidi, na ndio maana kila taasisi ya habari duniani na ndani inaongelea suala hilo.

"Wadau mbalimbali tunayodhima ya kuwekeza na kuwajengea uwezo wanahabari, kuhakikisha kwamba wanapata vifaa muhimu katika maeneo yako ya kazi, na shuleni, ili kuhakikisha kwamba tunapika waandishi wa habari wenye kujua teknolojia za kisasa za mitandao ya kidigitali," alisema Dk. Mukiza.

Aliongeza kuwa teknolojia isipotumiwa vizuri lazima italeta madhara, huku akisisitiza wadau katika sekta hiyo kutokubaki nyuma, badala yake waweke kipaumbele katika kutumia teknolojia ya kisasa ili kuifanya fursa ya mbadala wa yale yaliyokuwa yanairudisha nyuma tasnia ya habari.

Aidha, alieleza kuwa katika ulimwengu wa teknolojia taarifa zisizokuwa sahihi ziko, na kwamba kazi kubwa ya wanahabari ni kuona ni namna gani wanaweza kuukabili upotoshaji kupitia mitandao ya kijamii, ikiwemo kujikita kwenye mifumo inayoweza kuchanganua taarifa za uongo na ukweli 'Fact Cherk'.

Akihutubia kwa niaba ya Mkuu wa UDSM, Rais mstaafu Jakaya Kikwete, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknbolojia, Prof. Danieli Mushi, alisema ili kukabiliana na tatizo la kusambaa kwa taarifa za upotoshaji, ni muhimu wadau wa sekta hiyo kujikita katika kuzingatia maadili na kufanya tafiti zitakazosaidia kujua uhalijia wa jambo kwa undani.

"Vyombo vya habari vinatusaidia kwa kiasi kikubwa kuhamasisha masuala mbalimbali ya msingi ikiwemo utalii na uchumi wa buluu hali inayochagiza maendeleo ya kiuchumi, hivyo ni muhimu kuzingatia maadili na usahihi katika upashanaji habari pamoja na kuchochea ukuaji wa sekta hiyo," alisema Prof. Mushi.

Naye, Rais wa EACA, Prof. Margaret Jjuuko, alisema mkutamo huo unawapa fursa ya kushirikiashana mijadala mbalimbali inayotokana na tafiti na bunifu katika kukabili dhana potofu na namna ya kupaza sauti za jamii zilizotengwa.

Akichangia mada katika jukwaa hilo Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza la Habari la Tanzania (MCT), Ernest Sungura, alisema kuna haja ya serikali kushirikiana na wamiliki wa majukwa ya mitandaoni kuhakikisha maadili yanazingatiwa.

"Katika matukio ambapo kuna vitendo visivyo vya kimaadili, ni muhimu serikali kuingilia kati hivyo ushirikiano kati ya waanzilishi wa majukwaa na serikali itasaidia kuimarisha kanuni na uelewano bora," alisema.

Mkurugenzi wa Jukwaa la mtandaoni la JamiiForums, Maxence Melo, alisema ili kuhakikisha kuwa wanaipa kipaumbele jamii sauti zao kusikika walianzisha jukwaa lijulikanalo kama Fichua ambalo wanapata nafasi ya kueleza changamoto wanazokutana nazo bila ya majina yao kujulikana.

Alisema kupitia jukwaa hilo waandishi wa habari wanapata mawazo ya kihabari ambayo wanayeboresha na kutoa maandiko na kulete mabadiliko kwenye jamii.

Profesa Mirjam de Bujin wa Chuo Kikuu cha Leiden nchini Uholanzi alisisitiza wandishi wa habari kuwa na uhuru wa kuwajibisha serikali na kampuni pale wanapoenda kinyume na utaratibu.

## Watetezi mazingira kupanda miti milioni tano ya kahawa

**Na Christina Mwakangale**

WATETEZI wa mazingira duniani wanatarajia kupanda miche ya miti milioni tano ya kahawa katika Mkoa wa Kagera ili kutunza mazingira na kuongeza kipato cha wakazi wa eneo hilo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya BR Food kutoka nchini Brazil, Colin Francis, aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti 200 katika Shule ya Msingi Kerezange, jijini Dar es Salaam.

Alisema hatua hiyo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kulinda mazingira, hasa kwa kupanda miti ambayo huchangia kukabiliana na hewa ukaa.

"Miti milioni tano ya kahawa itapandwa katika hekta 1,000. Mradi huu unalenga kutunza mazingira, kuongeza kipato kwa wananchi kupitia biashara ya zao hili, ambalo lina soko duniani," alisema Francis.

Aina hiyo ya miche inastahimili hali ya hewa ya mazingira na pia upandaji huo umeanza mwaka huu na unatarajiwa kukamilika mwaka 2030.

"Brazil na Tanzania wanafanana viwango vya hali ya hewa, hivyo mpango huu wa kupanda miti kwa awamu hadi ifikapo 2030 tunatarajia utakuwa na matokeo chanya, kwa mazingira na uchumi kupitia biashara ya uuzaji wa zao, kaboni," alisema Francis.

Meneja Uwekezaji kutoka Wakala wa African Carbon, Ernest Mziray, alisema lengo la mradi huo ni utekelezaji wa sera ya 'A to zero' kupunguza hewa ukaa.

Alisema miti itakayopandwa itapunguza kiwango cha uchafuzi wa hewa, huku mradi huo ukienda sambamba na kuwahamasisha vijana kucheza mpira wa miguu wawapo shuleni.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kerezange, Job Ndubussa, aliwashukuru wadau hao akisema miongoni mwa sababu za shule hiyo kuchaguliwa kwa kampeni hiyo ni kutokana na kuwa mlinzi wa mazingira ikiwa imesheheni miti kwa ajili ya kivuli.

Alisema shule hiyo pamoja na kupanda miti, pia ilipokea zawadi za jezi kwa ajili ya michezo na mipira ya kuchezea mpira wa miguu kutoka kwa wadau hao.

Kilimo cha kahawa nchini kinawezesha maisha ya watu takribani 400,000 ikizalishwa katika wilaya 52 na kuchangia uchumi wa nchi, huku uzalishaji ukifikia Dola za Marekani milioni 100 kwa mwaka, ikiuzwa nchi ya Japan, Italia, Ujerumani na Marekani.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-28

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Materu alijifunza kitu kuwa mlinzi japo kuna baadhi ya wafanyakazi huwadharau kutokana na kazi zao za kukaa mlangoni, getini, kuuliza watu maswali, kufungulia geti magari, lakini ni watu muhimu kwenye ulinzi binafsi.

Kwa sababu, yoyote atakayefika pale na kumuuliza mtu ambaye humjali kwa kumuachia chochote kitu mara kwa mara, basi atapigwa maswali, halafu atawasiliana kwanza na mwenyewe kabla ya kumruhusu.

Hii imesababisha wengi kuepuka maadui zao, au watu ambao walikuwa wanataka kuja kuwadhuru.

Na hili ndilo limemfanya Materu awe hivyo. Anafanya hivyo kama kinga, kwani chochote kibaya kikitokea dhidi yake, watamtaarifu na yeye atajua jinsi gani ya kuepuka.

Siku ya pili alifanya hivyo hivyo. Lakini kabla hajapanda akawatania. “Naona mmepata mlinzi nwingine hapo.” Walinzi waligeuka. Halafu wakaangua kicheko. “Rafiki yetu huyu, yupo wiki ya pili sasa, mara anapita mara anakaa jirani hapo. Ila siyo mgomvi. Anakaa mwenyewe anaongea maneno yaliyoeleweka, halafu huyo anaondoka.” Akajibu mmoja wa walinzi.

Walikuwa wakimzungumzia mwendawazimu. Mita chache kutoka walipo, alikaa mwendawazimu mmoja aliyekuwa akila mikate mikavu. Kwake Materu ilikuwa ni mara ya kwanza kumuona, lakini kwa walinzi ilikuwa ni wiki ya pili. Ni kweli alikuwa akija pale, anasimama, mara anakwenda kukaa pembeni, na kuna siku anapita tu bila kusimama kama vile hapajui.


******************************

Alitafuta zaidi ya mara 10. Hakuna kilichobadilika. Ni kwamba hakukuwa na dalili hata ya miujiza kuwa angeweza kuviona. Macho yalimtoka pima. Hakujua nini afanye. Hakujua nani amuulize. Alionekana kuchanganyikiwa.

“Ni uchawi au?” Akajiuliza huku jasho lilikuwa linamtoka licha ya kwamba kulikuwa na kipoza joto kipya ambacho alikifunga mwezi mmoja uliopita.

Taratibu akarudisha kumbukumbu nyuma huenda kuna sehemu ambayo alikuwa ameweka. Lakini kila akifanya hivyo akili inamwambia kuwa hawajahi kuweka sehemu nyingi zaidi ya hapo.

Akaamua aangalie tena kwenye droo ambayo aliifunga, akaambulia tena patupu. Kitu kilichomshangaza ni kwamba droo ilikuwa imefungwa vile vile kama alivyofanya mara ya mwisho. Anakumbuka mara ya mwisho kuangalia flashi zake mbili zilizopotea ilikuwa ni wiki moja iliyopita. Flashi hizi alizilinda kama mboni ya macho yake. Alizilinda kama anavyolinda mali na biashara zake. Moja kati ya siri zake kubwa ambazo zingeweza kumharibia sifa zilikuwa kwenye flashi hizo mbili. Boniphace Materu alichanganyikiwa. Akajiuliza kama anaweza kwenda kuwauliza walinzi aliowaacha jana. Hata hivyo sauti nyingine ikamtuma kuwa asifanye hivyo kwani inaweza kumletea matatizo watu wakaanza kujua kitu gani amepoteza na hiyo itaanza kuwapa zoezi la kutaka kujua. Akaamua kukaa kimya kwanza, lakini pamoja na kuamua hivyo lakini alikuwa makini mno kwani hakujua nani aliyefanya hivyo na kwa sababu gani.




**“Ni lazima nimpate huku mtu ambaye ameingia ndani ya ofisi yangu na kuiba flashi hizi kaba hajaniharibia mambo yangu.” akaongea mwenyewe ofisini akiwa peke yake.**

Ni kwamba yoyote aliyefungua droo hakuwa mtu wa kawaida. Alifungua akiwa na ufunguo bandia. Hivyo akawa na wasiwasi kwamba huenda angeweza kuwa askari. Na kama kuna mtu aliingia ndani ya ofisi yake ni kwa nini aliamua kusaka flashi hizi mbili tu? Na alijuaje kama kuna flashi hizo kwenye droo hiyo? Ndani au ofisi yake kulikuwa na droo nyingi na flashi zisizo wa idadi, nyingi zikiwa ni kwa ajili ya kumbukumbu ya biashara zake.

Akashangaa kuona zile flasi za siri ya kampuni yake zilikuwepo kama kawaida. Zingine hazikuguswa. Kwa nini hizo tu? Hapo akagundua kuna kitu ambacho si cha kawaida kinachoweza kumpata mbele ya safari. Na inabidi alifanyia kazi. Ikiwezekana hata kuua watu zaidi ya 10 kwa ajili ya kuficha ukweli ambao ameendelea kuuficha kwa gharama nyingi.

Alichofanya akawapigia wadau wote ambao alikuwa akiwahonga kwa ajili ya kuuficha ukweli juu ya kupotea kwa flashi ambazo zimelinda siri ile, hivyo wamsaidie kumsaka yoyote atakayeonekana amezishikilia. Alipomaliza alihisi miguu kutetemeka. Akili ikamtuma kuwa inawezekana aliyefanya hivyo ni wapinzani wenzake kisiasa ambao nao walitaka jimbo moja la Kilimanjaro analotaka kugombea.

“Ni lazima nimpate huku mtu ambaye ameingia ndani ya ofisi yangu na kuiba flashi hizi kaba hajaniharibia mambo yangu.” akaongea mwenyewe ofisini akiwa peke yake.

Mlango ukagongwa. Akatembea kwa hatua za kivivu huku akiwa na mawazo, akafungua mlango. Aliyeingia ni mkuu wa ulinzi wa jengo. Kuingia kwake tu kulimpa picha kuwa kuna tatizo. Akamkaribisha huku akijilazimisha kutabasamu kama vile hakuna kilichotokea.

“Bosi habari.” “Nzuri mzee Maliki, mbona si kawaida yako kuvamia ofisi za watu mida hii?” Akauliza huku akitegemea kupata taarifa ambazo si za kawaida. “Bwana tuna taarifa kuwa walinzi wetu wawili jana walipigwa, wakanyang’anywa silaha ambazo aliyefanya hivyo hakuondoka nazo. Kwa sasa walinzi wale wamelazwa Hospitali ya Rufaa Muhimbili wakiwa kwenye hali mbaya.” Taarifa hiyo ilimthibitishia Materu kuwa aliyefanya hivyo ndiyo huo waliyeingia kwenye ofisi yake na kuchukua flashi zake. “Cha ajabu bosi, tulidhani kuwa watu waliofanya hivyo watakuwa wameingia kwenye jengo hili na kuiba pesa, mali yoyote, au nyaraka, lakini kila ofisi niliyoenda wanasema kwao kuko salama. Sasa najiuliza hawa majambazi ambao hawakutumia silaha yoyote walifanya hivyo kwa kutaka nini hasa?” Taarifa ya mzee Maliki iliongeza maumivu kwa Materu. Ni kama kitu nilichokuwa kikikata jeraha ambalo halijapona. “Sasa bosi ofisi yangu ni ya mwisho, nimezunguka kuja kuangalia kama waliingia kwako na wameiba kitu chochote.” “Hapana, mimi hawakuchukua chochote, kila kitu kipo sawa!” Materu akaongopa. Hakutaka ijulikane kuwa amechukulia flashi. Labda zingekuwa za kiofisi, lakini zile ni za binafsi ambazo ni siri ambayo haikutakiwa yoyote ajue, ndiyo maana akakataa. “Sasa hawa jamaa alikuwa walikuwa wanataka nini, kwa sababu wamewapiga walinzi wetu mpaka wakazimia. Halafu hawakufanya chochote wakaondoka, hawakuvunja wala nini. Nia yao ilikuwa nini?” “Labda kuna mmoja wao waligombana naye huko kwao mitaani, wakaja kulipa kisasi.” Materu akaendelea kuongopa. Ni uongo ambao si halisi, lakini angalau ulimpa ahueni mzee Maliki mkuu wa ulinzi wa jengo hilo. “Wakipona mnaweza kuwauliza vizuri, wanaweza kuwa walikuja kulipa kisasi, mwenzake akataka kumsaidia kwa sababu wana silaha, wote wakaishia kupigwa.”

“Ila inavyoonekana wana mafunzo ya kijeshi au ukakamavu kwa sababu hata hawa walinzi pamoja na kwamba wanajua kutumia silaha, lakini wana mafunzo maalum ya mapigano, nadhani waliwahiwa au wenzao walikuwa na mafunzo maalum. Ila nguvu yote waliyotumia imewashangaza wengi kuwa ilikuwa ni kuwapiga tu, siyo kuja kuiba chochote maana hawajachukua silaha, wala kuingia kwenye jengo ambalo lina mali, pesa na vitu vingi.” Akashangaa mzee Maliki.

HABARI MICHEZO

# MGUNDA : SIMBA QUEENS HASIRA ZOTE LIGI KUU BARA

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kufanya vibaya katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Kocha Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, amesema wanarejea nyumbani wakiwa na hasira ya kuhakikisha wanatetea ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu mpya wa 2024/2025.

Simba Queens ilimaliza katika nafasi ya nne katika mashindano ya CECAFA yaliyomalizika kwa wenyeji CBE ya Ethiopia kutwaa taji hilo baada ya kuwafunga Polisi Kenya bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Abebe Bikila ulioko Addis Ababa, Ethiopia juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda, alisema ili wapate nafasi ya kushiriki tena michuano hiyo ni lazima wachukue ubingwa wa Tanzania, hivyo wanarudi na kazi moja ya kupambana ili kulinda taji wanalolishikilia.

Mgunda alisema wachezaji wake walifanya makosa katika mechi ya juzi na wapinzani wao Kawempe Muslim Ladies ya Uganda walitumia mapungufu hayo kuwahukumu na hivyo kulala mabao 2-0.

"Kwanza kabisa namshukuru Mungu kwa yaliyotokea, katika mchezo wa mpira ukifanya makosa ya kujirudia unaadhibiwa, sisi wenyewe tumekosea na ndio sababu tukaadhibiwa, lakini tunarejea nyumbani kujiandaa kuhakikisha mwakani tunarudi tena katika mashindano haya ya CECAFA. Inauma, inagusa sana, lakini tumeyakubali matokeo tuliyoyapata," alisema Mgunda.

Aliongeza yeye na benchi lake la ufundi watayafanyia kazi mapungufu yote yaliyojitokeza na wanaamini kila kitu kitakwenda vizuri kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

Naye aliyekuwa Kocha wa timu hiyo, Sebastian Nkoma, alisema kukosekana kwa mshambuliaji tegemeo, Aisha Mnunka, ambaye ametoroka kikosini, katika mashindano hayo lilikuwa ni pengo ‚kubwa'.

"Huwezi kusema kukosekana kwa Aisha sio pengo, tunafahamu Aisha ni mchezaji mzuri na ambaye alikuwa akiisaidia sana timu, ni lazima timu ibembeleze wachezaji wazuri, wachezaji wakubwa," Nkoma alisema.

Nkoma alisema pia ili kujiandaa vyema na michuano hiyo, Simba Queens ilipaswa kwenda kuweka kambi katika mikoa kama Iringa au Manyara ili kuzoea hali ya hewa ya baridi inayofanana na Ethiopia.

JKT Queens ya Tanzania ndio walikuwa mabingwa wa CECAFA mwaka jana lakini walishindwa kwenda kutetea taji hilo baada ya kuvuliwa ubingwa wa hapa nchini na Simba Queens ambayo mwaka juzi ilifika hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, michuano iliyofanyika Morocco.

# Fountain yafunguka kilichowapa ushindi

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-0 ugenini, Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Mohamed Muya, amesema siri ya kupata matokeo mazuri ilitokana na kufanyia kazi mapungufu waliyoyabaini walipocheza dhidi ya Simba wiki iliyopita.

Fountain Gate FC ilikubali kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Simba.

Akizungumza na gazeti hili, Muya, alisema baada ya mechi dhidi ya Simba, alikaa na wachezaji wake hasa wale wa nafasi ya ulinzi na kuwaelekeza namna ya kupunguza makosa.

Muya alisema pia aliwataka wachezaji wake kuongeza umakini na utulivu wanapokuwa na mpira jambo lililowasaidia kutawala kwa muda mrefu mchezo huo.

"Ukiangalia hatukubadilisha kitu, wachezaji wale wale waliocheza dhidi ya Simba ndiyo hawa hawa waliocheza hapa, tulichofanya ni kuwaelekeza kupunguza makosa hasa eneo la ulinzi, ingawa hatukupunguza kwa asilimia zote, lakini unaona tulikuwa vizuri, na hawa Namungo tulishacheza nao mechi ya kirafiki wakati wa ‚pre season', hivyo tulikuwa tunajua tunakwenda kucheza na timu ya aina gani," alisema Muya.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Mwinyi Zahera, amekalia kuti kavu. Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema tayari vikao vimeshaanza kumjadili kocha huyo huku baadhi ya viongozi pia wakitakiwa wawajibike.

Namungo ilianza msimu kwa kuchapwa mabao 2-1 na Tabora United.

Naye Zahera alisema sababu iliyowafanya wapoteze mchezo wa juzi ni makosa ya kibinadamu ya wachezaji wake.

"Sisi tulikuwa tunashambulia, wenzetu walikaa nyuma na kusubiri kushambulia kwa kushtukiza, sasa tukipoteza mpira wachezaji wangu wanachelewa kukimbia nyuma kwa haraka kwenda kuziba mianya, hili ndilo lililotugharimu, lakini lingine tulikuwa na makosa mengi. Wachezaji wangu wameruhusu mabao mepesi," alisema Mkongomani huyo.



Kiungo wa Simba, Awesu Awesu (kulia), akijiandaa kumiliki mpira kwenye mazoezi ya timu hiyo ambayo inatarajia kukutana na Al Hilal ya Sudan katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

# Bosi Namungo aachia ngazi

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Klabu ya Namungo ya mkoani Lindi inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara umetangaza kuachana na Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Omari Kaya, imeelezwa.

Taarifa hiyo imetolewa ikiwa imepita siku moja baada ya timu hiyo kupoteza mechi ya pili mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ilichapwa mabao 2-0 na Fountain Gate ikiwa nyumbani.



Klabu hiyo imesema Kaya aliomba kujiuzulu nafasi hiyo na uongozi umeridhia maombi hayo.

„Uongozi unamshukuru Kaaya kwa muda wote alitumikia klabu hii kama Ofisa Mtendaji Mkuu wetu na tunamtakia kila la heri," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kipigo hicho ni cha pili mfululizo kwa Namungo wakiwa kwenye uwanja wa nyumbani wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.

Namungo ilianza msimu mpya kwa kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Tabora United.

Kikosi hicho kinachonolewa na Mkongomani Mwinyi Zahera, kitashuka tena ugenini Septemba 12, mwaka huu kuwakabili wenyeji Dodoma Jiji FC.

Simba iliyocheza mechi mbili inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi sita wakati Namungo na Kagera Sugar zinaburuza mkia.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### STERLING ATAJWA ARSENAL
ARSENAL inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Chelsea, Raheem Sterling, mwenye umri wa miaka 29, au winga wa Bayern Munich Mfaransa Kingsley Coman (28), baada ya kuombwa kuwanunua wote wawili siku mbili za mwisho za uhamisho. ***(Independent)***

### NEWCASTLE YAMTEMA GUEHI
KLABU ya Newcastle United inaelekea kusitisha juhudi za kumsajili mlinzi wa England, Marc Guehi, mwenye umri wa miaka 24, baada ya kuchoshwa na mazungumzo ya muda mrefu na Crystal Palace. ***(Sky Sports)***

### TONEY MAMBO MAGUMU
MSHAMBULIAJI wa England na Brentford, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 28, anakabiliwa hatari ya kuachwa katika hali ya kutatanisha huku muda wa uhamisho ukizidi kuyoyoma. (Mirror)

### OSIMHEN ANUKIA SAUDIA
KLABU ya Saudi Arabia, Al-Ahli ina matumaini ya kumsajili mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25, katika hatua itakayodidimiza matumaini ya Chelsea kumnasa mshambuliaji huyo wa timu ya taifa ya Nigeria. ***(Sportsport)***

### LIVERPOOL YAIBANIA FOREST
LIVERPOOL imekataa ofa ya fedha taslimu pamoja na mchezaji kutoka Nottingham Forest kwa ajili ya mlinda mlango wao wa Jamhuri ya Ireland, Caoimhin Kelleher, mwenye umri wa miaka 25. ***(Athletic)***

### SANCHO AKARIBIA CHELSEA
CHELSEA inakaribia kumnunua winga wa England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 24, lakini wamewasilisha masharti yao kwa Manchester United kabla ya kufanya uamuzi huo. ***(Teamtalk)***

### ÉDOUARD KUTUA IPSWICH
KLABU ya Ipswich inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa, Odsonne Edouard, mwenye umri wa miaka 26 kutoka Crystal Palace baada ya usajili wa mkopo wa mshambuliaji wa Chelsea na Albania Armando Broja (22), kugonga mwamba. ***(Standard)***

### ALMIRON AKWAMA FULHAM
KLABU ya Fulham haitamsajili kiungo wa Newcastle United mwenye umri wa miaka 30 kutoka Paraguay, Miguel Almiron. ***(Mail)***

### ZOUMA KITAELEWEKA SAUDIA
MLINZI wa West Ham Mfaransa Kurt Zouma, mwenye umri wa miaka 29, amekamilisha uchunguzi wa matibabu na anakaribia kukamilisha uhamisho wa awali wa mkopo kwenda kwa Al-Orouba ya Saudi Pro League. ***(Sky Sports)***

### ARAUJO ATAJWA CHELSEA
CHELSEA imemuuliza beki wa Benfica ambaye ni raia wa Ureno, Tomas Araujo, mwenye umri wa miaka 22. ***(Mirror)***

### GILMOUR KUBAKIA NAPOLI
KIUNGO wa Scotland, Billy Gilmour mwenye umri wa miaka 23, hataweza kuhamia Napoli msimu huu baada ya kiungo mpya wa Brighton, Matt O'Riley kuthibitishwa amepata jeraha baya katika mechi yake ya kwanza msimu huu. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MADRID YATAKIWA KUIMARIKA HARAKA

**Ni kauli ya Ancellotti baada ya timu yake kulazimishwa tena sare...**

**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema timu yake „lazima itafute maendeleo haraka „baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Las Palmas na kuachwa wakiwa nyuma kwa pointi nne dhidi ya vinara wa LaLiga, Barcelona.

Alberto Moleiro aliifungia Las Palmas dakika ya tano wakati Vinícius Júnior alisawazisha kwa mkwaju wa penalti kipindi cha pili, Madrid wakishikiliwa kwa mara ya pili katika mechi tatu za Ligi Kuu Hispania, kufuatia sare ya kwanza ya 1-1 dhidi ya Mallorca.

Kylian Mbappé alicheza dakika zote 90, akipiga mashuti tisa, mawili yakilenga goli, lakini hakufunga kwa mechi ya tatu mfululizo.

"Kilikuwa kipindi kibaya cha kwanza," alisema Ancelotti akikiri katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Ilikuwa ngumu kwetu kupata bao. Ilibidi tusubiri, tuteseke kidogo.

"Timu haikuwa na usawa, hatukusogeza mpira haraka. Ilikuwa ngumu kwetu kushinda mpira nyuma. Kila kitu kilichotokea katika sare dhidi ya Mallorca. Sikuona mabadiliko katika timu. Lazima tutafute uboreshaji haraka, na nadhani tutaipata."

Mabingwa hao wa Hispania walianza msimu huu kwa kushinda UEFA Super Cup kabla ya kuanza kampeni yao ya msimu wa 2024-25 wa LaLiga kwa kuangusha pointi mbili huko Mallorca.

Waliishinda Real Valladolid mabao 3-0 nyumbani Jumapili iliyopita, na baada ya sare ya Alhamisi huko Las Palmas, watakuwa wenyeji wa Real Betis hapo kesho Jumapili, kabla ya kusafiri kwenda Real Sociedad baada ya mapumziko ya kalenda ya kimataifa.

"Imekuwa vigumu kwetu kupata uimara tuliokuwa nao mwaka jana," alisema Ancelotti. "Hatuwezi kutafuta visingizio, tunatakiwa kuimarika kwa kasi, tuna mchezo mwingine Jumapili.

"Lazima niwe wazi zaidi katika mkakati wa uwanjani, ili kutoa ufafanuzi kwa wachezaji. Imekuwa ngumu kwetu kuliko tulivyofikiria... Michezo hii mitatu imenionyesha mambo mengi ambayo hayaendi vizuri."

Ancelotti alifanya mabadiliko manne kwenye timu yake dhidi ya Las Palmas, huku Lucas Vázquez, Ferland Mendy, Luka Modric na Brahim Díaz wakiingia, bila maboresho makubwa.

HABARI MICHEZO

# LIVERPOOL KUIKABILI REAL MADRID UEFA

**MONACO,** UFARANSA

LIVERPOOL imepangwa kuchuana na Real Madrid kama sehemu ya muundo wa mpya wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ulioboreshwa wa timu 36, huku Kocha Mkuu wa Barcelona, Hansi Flick, akirejea Ujerumani kumenyana na waajiri wake wa zamani, Bayern Munich.

Vigogo wa Ujerumani, Bayern watakutana na Barca katika shindano hilo kwa mara ya tatu katika misimu minne iliyopita.

Bayern Munich imeshinda mechi sita zilizopita, ikiwa ni pamoja na ushindi wa mabao 8-2 wa robo fainali katika njia yake ya kutwaa Ligi ya Mabingwa mwaka 2020 chini ya Flick.

Droo hiyo iliyofanywa na muunganiko wa Gianluigi Buffon, Cristiano Ronaldo na kompyuta ya juu zaidi ya UEFA, pia ilizua pambano la uzito wa juu likiwamo la Manchester City dhidi ya Paris Saint-Germain na marudio ya fainali ya mwaka jana kati ya Borussia Dortmund dhidi ya Real Madrid.

Arsenal walifanikiwa kuzikwepa baadhi ya timu ngumu walipopangwa kucheza dhidi ya PSG na Inter Milan wakati Aston Villa watamenyana na Bayern kwa mara ya kwanza tangu walipowafunga wababe hao wa Bundesliga katika fainali ya Kombe la Ulaya mwaka 1982.

Pamoja na kuwakaribisha Real Madrid, Liverpool pia itaungana na kiungo wa zamani Xabi Alonso atakapoipeleka timu yake ya Bayer Leverkusen kuke Anfield.

Alonso alihusishwa sana na kibarua cha ukocha katika klabu ya Liverpool baada ya tangazo la kushangaza la Jürgen Klopp Januari atajiuzulu nafasi hiyo.

Katika mfumo mpya wa mashindano haya, kila timu itacheza michezo nane kabla ya michujo -- miwili zaidi ya miaka iliyopita -- huku duru ya mwisho ya mechi ikifanyika Januari 29, mwakani.

Kila timu itacheza mechi nne nyumbani, na nne ugenini.

Timu kutoka ligi moja hazikupangwa dhidi ya kila mmoja, na kila klabu inaweza kucheza si zaidi ya timu mbili kutoka nchi moja.

Timu nane bora zitatinga hatua ya 16 moja kwa moja. Timu zitakazomaliza kati ya tisa na 24 zitafuzu kwa hatua ya mtoano, huku zile 12 za chini zikitolewa.

# Majeruhi yamchanganya Mount

**MANCHESTER,** ENGLAND



KIUNGO wa kati wa Manchester United, Mason Mount, amekuwa nje ya uwanja kwa mechi chache kutokana na jeraha dogo la misuli, klabu hiyo ya Ligi Kuu England imesema.

Mshambuliaji, Rasmus Højlund na mabeki Luke Shaw, Leny Yoro, Tyrell Malacia, na Victor Lindelof pia watakuwa nje kutokana na majeraha kabla ya mchezo wa ligi dhidi ya Liverpool utakaochezwa kesho kwenye Jumapili Uwanja wa Old Trafford.

Mount alianza mechi zote mbili za ligi za United msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye alitolewa wakati wa mapumziko katika kichapo cha mabao 2-1 wikendi iliyopita dhidi ya Brighton & Hove Albion, alisema alipata jeraha hilo wakati wa mechi.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea alisajiliwa na United Julai mwaka, 2023 kwa takriban pauni milioni 55, lakini alicheza mechi 20 pekee msimu uliopita kutokana na majeraha mengi.

"Wakati wa mchezo uliopita nilipata tatizo dogo la misuli," aliandika Mason kwenye mtandao wa kijamii. „Nimeiangalia na inaonekana kama nitakuwa nje kwa mechi chache."

Mount alipata jeraha la misuli ya paja msimu uliopita Agost na Novemba, mwaka jana alikaa nje kwa miezi minne kutokana na jeraha la mguu na kufanikiwa kucheza mechi nane zaidi.

„Kuongoza kabla na wakati wa maandalizi ya msimu, nilijitahidi sana kurudisha utimamu wangu pale inapohitajika na nilihisi nikiwa na nguvu, mkali na tayari," aliongeza Mason.

"Nilitaka usikie moja kwa moja kutoka kwangu jinsi nilivyochanganyikiwa, kama ninavyotarajia wewe pia. Nitafanya kila liwezekanalo kurejea katika hali bora na kuisaidia timu."

Nyota huyo wa kimataifa wa England hakutajwa katika kikosi cha Kocha wa muda Lee Carsley, ambacho kitacheza na Ireland huko Dublin Septemba 7, mwaka huu na Finland huko Wembley siku tatu baadaye katika Ligi ya Mataifa ya Uefa.




# Ronaldo: Nitarudi kuchezea UEFA

**MONACO,** UFARANSA

NAHODHA wa Al Nassr, Cristiano Ronaldo, ameacha milango wazi siku moja atarejea kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Sporting, Manchester United, Real Madrid na Juventus alitunukiwa tuzo ya Mfungaji Bora wa muda wote katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa na mabao 140 kwenye mashindano hayo.

Ronaldo na Gianluigi Buffon walikuwa jukwaani huku droo ya kwanza chini ya muundo mpya ikifanyika huko Monaco.

Alipodhihakiwa na Rais wa UEFA, Aleksander Čeferin, Ronaldo alisema kuna siku moja atarejea.

„Nacheza Ligi ya Mabingwa ya Asia, usisahau hilo," alisema Ronaldo.

„Kwangu mimi ni furaha kuwa hapa. Asante kwa tuzo hii ya ajabu ina maana kubwa kwangu," aliongeza Ronaldo.

"Kama unavyojua, Ligi ya Mabingwa Ulaya ndiyo kiwango cha juu zaidi katika soka, nilipata nafasi, si unajua tu rekodi inajieleza yenyewe, lakini simaanishi hivyo, namaanisha furaha kucheza mashindano hayo... ni motisha yetu. .

„Kwenye soka huwezi kujua nini kitatokea, wacha tuone siku zijazo zitaleta nini."

Alinyanyua taji hilo mara tano, mara moja akiwa na United na mara nne akiwa na Madrid.

HABARI MICHEZO

# MOROCCO AFURAHISHWA ARI MAZOEZI TAIFA STARS

**Adam Fungamwango na Shufaa Lymo**

KUELEKEA mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika dhidi ya Ethiopia, Kaimu Kocha Mkuu wa Timu ya Tanzania (Taifa Stars), Hemed Suleiman 'Morocco' amesema anafurahishwa na morali na ari ya wachezaji wake.

Taifa Stars itaikaribisha Ethiopia katika mechi ya Kundi H itakayochezwa Septemba 4, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Morocco aliliambia gazeti hili wachezaji wake wamekuwa wepesi katika kupokea maelekezo kitu ambacho kinampa moyo wa kupata matokeo mazuri kwenye mechi hiyo.

Kocha huyo alisema pia kila mchezaji anaonekana ana kiu ya kupata nafasi ya kucheza na kuipambania nchi yake na hiyo inawaongezea nguvu kwenye kikosi hicho.

"Mazoezi yanaendelea vizuri, na wachezaji wote kwa mujibu wa madaktari wako fiti kwa sababu walipimwa afya walipowasili, nimefurahi sana kwa sababu wamekuwa wepesi ya kushika kile ambacho wanaelekezwa, huu ni mwanzo mzuri na kwa hiki nilichokiona kinanipa matumaini ya kuwafunga Ethiopia.

Kwa vyovyote vile katika mchezo wa kwanza ni lazima tupate ushindi kwa sababu tunacheza nyumbani, pili ndiyo mchezo ambao utatupa mwanga wa kuangazia kule mbele tunakokwenda," alisema Morocco.

Aliongeza hana wasiwasi kwa wachezaji wake kucheza michezo miwili kwa tarehe zinazokaribiana kwa sababu hii si mara ya kwanza kalenda ya mashindano hayo kuwa hivyo.

"Ukweli wachezaji wangu wameshawahi kufanya hivyo mara kadhaa katika michuano mbalimbali iliyopita, haiwezi kutuathiri, tunacheza hapa, halafu tutasafiri kwenda kucheza dhidi ya Guinea kwa nguvu ile ile," aliongeza Morocco.

Kocha huyo amewataka mashabiki wa soka nchini kujitokeza kwa wingi kuishangilia Stars ili ianze kwa kupata ushindi hapa nyumbani.

„Naomba Watanzania waje kwa wingi, naamini watakuja, tunatakiwa tushinde mechi hii kwa mazingira yoyote yale ili tuwe na mwanzo mzuri," alisema Mzanzibari huyo.

Baada ya mechi ya Jumatano, Stars itaifuata Guinea kwa ajili ya mchezo mwingine wa Kundi H utakaochezwa Septemba 10, mwaka huu.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Iboni iliyoko katika Wilaya ya Kondoa mkoani, Dodoma wakicheza mpira wa miguu wakati wa mapumziko kwenye uwanja wa shule hiyo hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Coastal Union yachekelea sare

**Na Adam Fungamwango**

COASTAL Union imesema mapumziko mafupi ya Kalenda ya FIFA kwao yamekuja wakati mwafaka ambapo watayatumia kuimarisha benchi la ufundi baada ya kumtimua Kocha Mkuu, David Ouma lakini ikifurahia sare waliyopata ugenini dhidi ya KMC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa juzi.

Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El Sabri, alisema kikosi chao kwa sasa kinahangaika kupata muunganiko ambao ndiyo unawasumbua na matokeo ya sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC kwao ni kama ushindi.

"Sisi tunahangaika na muunganiko kwa sababu tuna wachezaji wengi wapya, nadhani kila michezo itakavyozidi kusonga mbele tutaimarika, tulipoteza CECAFA, baada ya Ngao ya Jamii, tukaenda kufungwa na Bravo do Maquis, mechi ya pili tukaanza kutoka suluhu ya bila kufungana, hii inaonyesha haturudi chini ila tunapanda juu, na mapumziko ya FIFA, yatatusaidia kuimarisha timu," alisema El Sabri.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema wakati wowote watamtangaza kocha mpya raia wa Uganda.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moallin, aliliambia gazeti hili waliikamata mechi lakini wakashindwa kuimaliza.

"Nimeridishwa na viwango vya wachezaji wangu, kusema kweli bado ni mapema, wanahitaji muda, tulitawala mpira lakini hatukuimaliza mechi na nimewaambia kuwa tunapaswa kujifunza kutokana na hili, tunatakiwa kufanya zaidi ya hivi," alisema Moallin.

## Gamondi: Hatujacheza vizuri

INATOKA UK. 24

hautakuwa mwepesi, tulijua Kagera Sugar hawatakuwa wepesi kwenye uwanja wao wa nyumbani, tunashukuru lengo la ushindi limetimia,"alisema Gamondi.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa Yanga ambayo ilikuwa inashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini ulikuwa ni mchezo wa pili kwa Kagera Sugar.

Ushindi huo umeifanya Yanga kutopoteza mechi ya raundi ya kwanza kwa misimu 10 mfululizo tangu msimu wa mwaka 2014/2015.

Mara ya mwisho Yanga kupoteza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ni Septemba 20, 2014 ilipofungwa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani, Morogoro dhidi wenyeji Mtibwa Sugar, mabao yaliyofungwa na Mussa Hassan 'Mgosi' na Ame Ally.

Simba ndio vinara wa ligi hiyo yenye timu 16, akiwa na pointi sita baada ya kushinda mechi zote mbili walizocheza sawa na Singida Fountain Gate huku Mashujaa FC ya Kigoma ikiwa kwenye nafasi ya tatu na pointi zake nne kibindoni wakati Yanga inafuatia ikiwa na pointi tatu.

Fountain Gate ya Singida iliyopanda daraja msimu huu inafuatia katika msimamo huo ikiwa na pointi tatu sawa na Tabora United ya mkoani Tabora.

Kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha kalenda ya kimataifa ambapo hapa nchini Taifa Stars itawakaribisha Ethiopia katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Simba, Al Hilal kujiuliza

INATOKA UK. 24

Fadlu.

Aliongeza pia atatumia mechi hiyo kuwapa nafasi wachezaji wengine ambao hawakutumika kabisa kwenye mechi mbili za Ligi Kuu walizocheza ili wawe na utimamu wa mwili vizuri.

Simba itaanza kutupa karata yake katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika ugenini Septemba 13, mwaka huu dhidi ya Al Ahly Tripoli huku mchezo wa marudiano utafanyika wiki moja baadaye kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Jumamosi Agosti 31, 2024

## Madrid yatakiwa kuimarika haraka

UKURASA 21





# Gamondi: Hatujacheza vizuri

●●●Kocha huyo alalamika wachezaji wake walipoteza nafasi nyingi...

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya kuanza vyema kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuvuna pointi tatu muhimu dhidi ya wenyeji Kagera Sugar, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamodi, amesema timu yake haikucheza vizuri.

Yanga iliichapa Kagera Sugar mabao 2-0, mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani, Kagera juzi.

Akizungumza na gazeti hili, Gamondi, alisema ameshangazwa wachezaji wake kupoteza nafasi nyingi za kufunga katika mchezo huo ambao ulikuwa kiporo kwa sababu ya mabingwa hao kuwa kwenye majukumu mengine ya kimataifa.

Gamondi alisema kama wachezaji wake wangeongeza utulivu, wangeibuka na ushindi mnono na kujiwekea ‚mtaji' kuelekea kwenye mbio za ubingwa ambazo wameanza.

"Nadhani kama tungekuwa makini tungepeta ushindi mkubwa zaidi, hatukuwa vizuri mwenye umaliziaji, tumepoteza nafasi nyingi sana," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema walipoteza zaidi umakini katika dakika 25 za mwisho za mechi hiyo ya raundi ya kwanza.

„Hatupaswi kufanya hivi tena, tutalifanyia kazi kwenye uwanja wa mazoezi, ni muhimu kutumia vizuri nafasi nyingi tunazozipata, muda mwingine mchezo unabadilika kwa sababu wapinzani nao pia huwa wanatafuta matokeo mazuri, lazima tuwe makini, „ Gamondi alisema.

Aliongeza kikubwa wanachokifurahia ni matokeo chanya waliyopata kwenye mchezo huo wa ugenini.

„Lengo letu lilikuwa ushindi, tunafurahi tumepata ushindi kwa sababu pamoja na yote, tulijua mchezo huu

INAENDELEA UK. 23

Winga wa Yanga, Maxi Nzengeli (kushoto) akishangilia pamoja na Pacome Zoazoua baada ya Mkongomani huyo kufunga bao la kwanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mkoani Kagera juzi. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON) dhidi ya Ethiopia itakayochezwa Septemba 4, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Simba, Al Hilal kujiuliza

**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA kulala, ndio kinachoonekana kwa wawakilishi wa Tanzania Katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba ambao wanatarajia kuikaribisha Al Hilal ya Sudan katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Hata hivyo, katika mchezo wa leo, Simba huenda ikamtambulisha straika wake mpya, Leonel Ateba, ambaye alikuwa nyota wa mwisho wa kimataifa kusajiliwa.

Ateba, hajaonekana katika michezo miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo Wekundu wa Msimbazi wamecheza dhidi ya Tabora United na Fountain Gate kutokana na kukosekana kwa vibali.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amewaambia mashabiki kwa timu hiyo leo itakuwa ni nafasi nzuri kumwona mchezaji huyo kwa mara ya kwanza kwa sababu atamtumia, huku pia akiendelea kumpa nafasi straika wa Mtanzania, Velentino Mashaka, ameshapachika mabao mawili.

Fadlu alisema Mashaka ameanza kumpa mwangaza mzuri na anaamini ataendelea kuwa ‚moto'.

"Ateba kesho (leo) ndiyo atakayeongoza mashambulizi kwa sababu nataka nimwone kwa uzuri zaidi katika mchezo mkubwa kama huu, nadhani na mashabiki nao watapata fursa ya kumwona baada ya kukosekana mara mbili, lakini pia kuna Valentino, naye atapata nafasi, ni kijana mzuri ambaye katika mechi zote mbili amefunga bao moja akitokea benchi. Mukwala naye itategemea kama akichelewa kwenda katika kikosi cha taifa atacheza, lakini kama akiondoka mapema hatakuwepo," alisema

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >